SportPesa
TZS. 1,013,643,920
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Watanzania** waliokwama nchini Ukraine waondoka salama

UKURASA 2



**MODRIC AMTAKA MBAPPE MADRID**

UKURASA 22

Nipashe
Alhamisi Machi 10, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580880
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Mbowe akoleza wimbo wa siasa za kiungwana

• **Ateta** na RC Iringa na kuafikiana, asema walichoteta na Samia Ikulu kiheshimiwe... *Endelea ukurasa 2*



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga (katikati), akimkaribisha kwa furaha Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, alipomtembelea ofisini kwake, mjini Iringa jana, kwa ajili ya mazungumzo. Kushoto ni Mwenyekiti wa Baraza la Wazee la chama hicho, Suzan Lyimo. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**HATUA ZAANZA RASMI KUKABILI VIWAVIJESHI**
WIZARA ya Kilimo imetoa tahadhari ya uwapo wa wadudu waharibifu wa...

UKURASA WA 3
**WAELEZA ATHARI UCHUMI VITA RUSSIA NA UKRAINE**
SIKU moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutahadharisha kuwa ugumu...

UKURASA WA 7
**KORTI YAKATAA VIDEO MAUAJI DADA BIL. MSUYA**
MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imekataa kupokea kielelezo cha...

## Udanganyifu wa mitihani kupatiwa dawa ya kudumu

UKURASA 3



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store



## TANESCO kuja na mfumo mpya uuzaji umeme LUKU

UKURASA 2

MICHEZO **SIMBA YAONGEZA MAKALI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA




Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi (kushoto), akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 30 kwa niaba ya Zanzibar Maisha Bora Foundation kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, jijini Zanzibar, kwa ajili ya kusaidia kinamama hususani wale wanaojihusisha na kilimo cha mwani na chumvi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbowe akoleza moto siasa za kiungwana

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ameendelea kukoleza moto kuhusu kuwapo kwa siasa za kiungwana na kistaarabu zenye misingi ya kudumisha amani, upendo na mshikamano.

Mbowe, jana alifika ofisini kwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga na kufanya mazungumzo na wawili hao walikubaliana kufanya siasa za kistaarabu mkoani hapo. Mazungumzo hayo yalihudhuriwa pia na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi (ACP) Allan Bukumbi.

Akizungumza baada ya kufanya mazungumzo na Sendiga, Mbowe alisema kama ambavyo alizungumza na Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu jijini Dar es Salaam baada ya kutoka gerezani, anaona ni vyema kuendelea kueneza ujumbe wa siasa za kistarabu ili kukuza demokrasia.

"Tulikuwa kwenye mkoa wenu wa Iringa na tumemaliza uwapo wetu kwa usalama ndani ya mkoa huu. Tunashukuru na tumeona ni vizuri kukutana na viongozi wa serikali ya mkoa huu," alisema.

Mbowe alisema mambo ambayo alizungumza na Rais Samia juu ya kuijenga Tanzania na mambo ambayo yanapaswa kuzungumzwa kila wakati na kila mmoja wetu kuona siasa zonazofanyika zinakuwa za kistarabu na zenye upendo na mshikamano badala ya kufanya siasa za ugomvi na uhasama.

Kiongozi huyo alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Sendiga, kwa kukubali kumkaribisha ofisini kwake na kufanya nae mazungumzo hayo.

Sendiga kwa upande wake alimpongeza Mbowe kwa kufika ofisini kwake na kubainisha kuwa ofisi yake ni ya umma, hivyo inampokea kila mmoja na kuwa busara zake za kufika ofisini ni wazi anahitaji taifa lenye siasa safi.

Alisema Mbowe amemwomba kuendelea kufanya siasa safi ndani ya mkoa na yeye kwa nafasi yake ya mkuu wa mkoa, amemhakikishia kufanya siasa safi zenye tija kwa ustawi wa taifa.

Alisema Mkoa wa Iringa utaendelea kudumisha siasa safi zenye maendeleo kwa kuwa suala la amani na utulivu ni msingi mkubwa wa maendeleo ya mkoa na taifa.

"Naamini Mbowe huu ndio mkoa wake wa kwanza kuutembelea na kuja kukutana na mkuu wa mkoa. Niseme ni mwanzo mzuri na sisi mkoa tupo kuona amani inadumishwa," alisema Sendiga.

Hata hivyo, Sendiga aliwaomba viongozi wa vyama vya siasa mkoani Iringa kufanya kazi Kwa ushirikiano kwa kufanikisha kwa pamoja kuujenga mkoa na pale penye changamoto, wasisite kumshirikisha badala ya kukimbilia kwenye mitandao ya kijamii.

# TANESCO yaja na mfumo mpya wa kununua umeme

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) limesema kuanzia Julai mwaka huu litakuwa na mfumo wa ununuzi wa umeme ambao utawezesha wateja wao kuweka umeme kwenye mita papo hapo (automatically) tofauti na wa sasa unaohitajika 'token' kuingizwa kwenye mita zao.

Mkurugenzi wa TEHAMA wa shirika hilo, Cliff Maregeli, alibainisha hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu mfumo huo unaotarajiwa kuanza na majaribio kwa kubadili mita na kuweka mpya zenye uwezo wa kusoma mfumo wa TANESCO.

Maregeli alisema kwamba mita zilizopo sasa hazina mfumo wa kisasa kubaini masuala mbalimbali ikiwamo eneo ambako umeme umekatika au mteja amekosa huduma kutokana na kuchelewa kulipia huduma.

"Mita tulizonazo sasa hivi hazina uwezo wa kuongea na mifumo ya TANESCO. Sasa ukinunua umeme utahitajika kutafuta njia ya kuufikisha umeme nyumbani kwako. Tunakuja na njia ambayo tumeweka, tukikupa wewe inajua hiyo token ni ya kwetu.

"Sasa hivi shirika linakuja na mfumo wa mitajanja, tutaweza kufanya vitu vingi katika mfumo huu, utaweza kununua umeme wa shilingi 2,000 na 'automatically' (moja kwa moja) utaingia kwako," alisema Maregeli.

Alibainisha kuwa mradi huo upo kwenye hatua ya kukamilishwa na utaanza kwa majaribio kwenye maeneo yaliyo na watumiaji wengi wa huduma hiyo.

"Tutachagua eneo kama sehemu ya majaribio kwa kubadili mita zote na wateja waanze kutumia mfumo huu. Eneo kamili utaanzia wapi bado haijapangwa lakini miradi mingi ya aina hii huanzia kuliko na wateja wengi wa TANESCO, mfano Dar es Salaam," alisema.

TANESCO ni shirika la umma lililoanzishwa mwaka 1964 likiwa chini ya usimamizi wa wizara yenye dhamana ya nishati nchini.

# Watanzania waliokwama Ukraine waondoka salama

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema kundi la mwisho la wanafunzi 32 waliokuwa wamekwama katika mji wa Sumy, nchini Ukraine, limeondoka kwa mabasi kwenda miji ya Poltavo na Lviv nchini humo, kisha kuingia Hungary na Poland.

Hatua hiyo inakuja siku chache baada ya mmoja wa wanafunzi kuhojiwa na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) na kueleza madhila wanayopitia kuwa walifika mpakani wakarudishwa chuoni.

Mwanafunzi huyo alibainisha kuwa maisha ni magumu kwa kuwa hakuna maji, hivyo hawajaoga siku tatu, hawana chakula na wameshaishiwa fedha.

Pia alisema baadhi ya wanafunzi wa nchi zingine wameshaondolewa kwa mabasi hivyo akaiomba serikali kutumia balozi za jirani kuwasaidia waondoke nchini humo kwa kuwa walikwenda hadi mpakani na kurudishwa.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano Serikalini wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Emmanuel Buhohela, ilisema hatua hiyo imefikiwa baada ya mazungumzo yaliyofanyika kwa simu kati ya Waziri Liberata Mulamula na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Dmytro Kuleba, Machi 7, mwaka huu.

Ilisema aliiomba serikali ya Ukraine kusaidia kuwatoa Watanzania wanaosoma chuoni humo na kwamba aliridhia ombi la kuwasaidia wanafunzi waondoke salama kupitia mipaka ya Poland na Hungary kwa utaratibu ulioratibiwa na ubalozi wa Tanzania katika nchi za Sweden, Ujerumani na Russia.

"Wanafunzi wengine 61 wa chuo cha Sumy alfajiri juzi, 50 kati yao wanatarajia kuingia Hungary na 11 Poland. Maofisa wa Balozi za Tanzania nchini Sweden na Ujerumani wako tayari kwenye mipaka hiyo kwa ajili ya kuwapokea watakapowasili.

"Wanafunzi 11 waliotoka chuo cha Sumy kupitia njia salama iliyotolewa na serikali ya Urusi wamefanikiwa kuingia Urusi na tayari wamepokelewa na Ubalozi wa Tanzania ulioko Moscow, Russia," alisema.

Balozi huyo alisema balozi za Tanzania nchini Sweden na Ujerumani zimetoa namba maalumu kuwawezesha wanafunzi hao kuwasiliana na maofisa ubalozi watakapowasili mpakani.

"Kwa hatua hiyo, tunapenda kuwaarifu Watanzania wote kuwa hivi sasa hakuna mwanafunzi kutoka Tanzania aliyebaki kwenye chuo cha taifa cha Sumy kilichoko Ukraine,"alisema.

# Hatua zaanza rasmi kukabili viwavijeshi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imetoa tahadhari ya uwapo wa wadudu waharibifu wa mazao aina ya viwavijeshi, huku ikitoa lita 100,000 za dawa nchini ili kupambana na wadudu hao.

Akizungumza wakati akikagua mashamba yaliyoanza kuathiriwa na wadudu hao wilayani Chamwino, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema zaidi ya hekta 70,000 za mahindi wilayani humo zimeanza kushambuliwa na wadudu hao.

"Kutokana na hekta 70,000 za mahindi kuanza kushambuliwa na viwavijeshi kwa Chamwino tumetoa lita 200 za dawa na zitatolewa bure kwa wakulima kwa ajili ya kupulizia wadudu hawa, kwa sababu ni jukumu la serikali ni kupambana na viwavijeshi na wakulima kazi yao ni kulima na kununua mbegu na mbolea."

"Baada ya serikali kupata taarifa ya uwapo wa viwavijeshi, imeona haiwezi kumwachia mkulima jukumu la kununua dawa ya kuua viwavijeshi, mkulima anapaswa kununua mbegu na mbolea," alisema Bashe.

Alisema mpaka sasa halmashauri 39 zimekabiliwa na tatizo la viwavijeshi ikiwamo Chamwino na kuwataka wakurugenzi na maofisa ugani kuhakikisha dawa hizo zinamfikia na kumsaidia mkulima.

"Tunatambua sio kila mkulima atakuwa ana bomba kwa ajili ya kupulizia dawa, hivyo maofisa ugani wanapaswa kuwasaidia wakulima namna ya kutumia kuzipulizia," alisema.

Kuhusu mapigano ya Russia na Ukraine, Bashe alisema nchi hizo ndio wazalishaji wakubwa wa mbolea na kuwataka wakulima kutokuwa na haraka ya kuuza mazao kwa sababu serikali haijafunga mipaka.

"Sisi hatutakuzuia kuuza mwezi wa Juni na Julai ukivumilia unaweza kupata bei nzuri kidogo lengo ni kutaka mkulima mdogo asipate hasara," alisema Bashe.

Akizungumzia kuhusiana na suala la mbegu, Waziri huyo alisema wanatarajia kutoa tani 5,000 za mbegu za alizeti msimu ujao wa kilimo na watawauzia kwa bei ya Sh. 3500 kama bei ya ruzuku.

Naye Ofisa wa Kilimo wa Halmashauri ya Chamwino, Living Kilewe, alisema ugawaji dawa hizo katika mashamba yaliyoathiriwa umeanza ili kuzuia uharibifu wa zaidi ya hekta 70,000.

# Mfumo kudhibiti udanganyifu mitihani kuanza

**Na Salome Kitomari**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema imekamilisha mfumo wa usahihishaji mitihani kielektroniki uliotengenezwa nchini kwa zaidi ya Sh. milioni 550, utakaoanza kutumika vyuo vya ualimu, kwa lengo la kudhibiti uvujaji wa mitihani.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Prof. Adolf Mkenda, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kueleza mafanikio ya jumla.

"Mfumo umeundwa na Watanzania wenzetu ni wa kwanza barani Afrika, kila msahihishaji atakuwa na kishikwambi au kompyuta atasahihisha swali moja, litakaguliwa na mwingine na kisha kuhakiki na kuwekewa alama pasipo yeye kujua jina la mwanafunzi na namba," alisema.

Alisema lengo la mfumo huo ni kupunguza makosa ya usahihishaji na kwamba wanajivunia mfumo huo kwa kuwa zamani ili kuunda ililazimika kutumia wataalam kutoka nje, lakini kwa sasa ni Watanzania wenyewe.

**SHULE ZA VIPAJI**

Alisema kuanzia sasa atafuatilia kwa karibu wanafunzi wanaopangwa kwenda kusoma shule za vipaji maalum kwa kupitia jina kwa jina baada ya Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), kuwapanga kwenye shule hizo. "Wakishafanya uchaguzi wa wanafunzi nitaingia kuangalia jina moja hadi jingine kama ndiyo wanaostahili kusoma kwenye shule hizo, nikikuta kuna mtu kachomeka mwanawe au mtu wake bila vigezo nitamuondoa na kumweka mwenye sifa, nitakuwa mkali kwenye hili," alisema.

**MITAALA**

Aidha, Waziri Mkenda alisema wanaendelea na mapitio ya mitaala, na kwamba kwa sasa timu ya wataalam ipo mkoani Morogoro kufanya uchambuzi ili kutoa rasimu itakayopelekwa kwenye kongamano la wadau Mei, mwaka huu.

"Tunapitia mitaala na sera zetu, bado tuna mjadala kuwa muda wa kusoma uwe ni hadi darasa la saba au darasa la 10, je miundombinu na walimu itakuwaje, hatutaki kwenda kwa wadau tukiwa watupu bali na rasimu yetu ili tuijadili na kuboresha ili kuwa na nyaraka iliyoshirikisha wadau wote itakayokwenda kwenye mchakato wa kiserikali," alisema.

Alisema wizara haitaki kuamua yenyewe na ndiyo maana imefungua milango kwa wadau wote wa serikalini, binafsi na wananchi wa kawaida kutoa maoni ya muundo wa elimu kama unakidhi mahitaji ya sasa, namna gani tutawaondoa watoto kwenye kukariri mambo ambayo mengine hawayatumii kokote.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda (katikati), akiangalia bidhaa mbalimbali zilizotengenezwa kutokana na mabaki ya mazao zilizotokana na utafiti mbalimbali uliofanywa na Chuo Kikuu Ardhi (ARU), kabla ya kufungua mkutano wa kimataifa kuhusu ardhi, mazingira na mabadiliko ya tabianchi, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE.**

# Wachumi waanika athari za kiuchumi vita Russia, Ukraine

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutahadharisha kuwa ugumu wa maisha huenda ukatokea kutokana na vita vinavyoendelea kati ya Russia na Ukraine, wabobezi wa uchumi nchini wamekiri uwekezano wa baa hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini nchini (REPOA), Dk. Donald Mmari, akizungumza na Nipashe alisema taifa kubwa linavyoingia kwenye vita athari duniani inakuwapo kwa sababu ya vikwazo vinavyowekwa.

"Russia ni nchi ambayo inachangia kwenye uzalishaji wa mafuta duniani na bei yake ni nyeti, hivyo kwa kuwa na mapigano na nchi inayohusika kwenye uzalishaji mafuta inawezekana mafuta yanayozalishwa na kuingizwa sokoni yakapungua," alisema.

Alisema endapo Russia itashindwa kufikisha mafuta sokoni kutokana na vikwazo au sababu nyingine za kivita maana yake yatapungua na bei itapanda hasa kutokana na uchumi duniani ulikuwa umeanza kuondoka kwenye matatizo ya UVIKO -19 na uzalishaji uliongezeka na mahitaji ya nishati yaliongezeka.

"Bei ilianza kupanda hata kabla ya vita, sasa ukiingiza suala la vita uzalishaji unaweza kupungua na kiwango cha mafuta sokoni kitapungua maana yake bei itapanda.

"Jambo la pili, uchumi wa dunia unafungamana kwa mfano sekta ya utalii tukiangalia kuna watalii wanakuja Tanzania kutoka Russia, Ukraine na nchi nyingine zinazozunguka maeneo yale ambapo huenda huduma za usafiri zinaweza kuathirika.

"Maana yake itapunguza idadi ya watalii wanaokuja na fedha za kigeni zitapungua na kuleta nakisi kwenye bajeti na kwenye mizania ya fedha za kigeni, kwa maana ya mauzo ya nje na mahitaji ya bidhaa kutoka nje."

Dk. Mmari alisema inapotokea hayo, kuna uwekezano wa mfumuko wa bei kuwapo hasa katika uzalishaji na uchukuzi, ambao unategemea nishati ya mafuta ambapo ukipanda gharama zitaongezeka na za bidhaa nazo zitaongezeka.

"Hili ndilo angalizo ambalo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alilizungumza na ni jambo ambalo hatuna namna ya kulizuia, kwa sababu vita tayari inaendelea na namna ya kuzuia ni kushirikiana na mataifa mengine kuona kwamba vita vinakomeshwa, kusitishwa ili athari za kiuchumi zisiendelee," alisema.

Mchumi mbobezi, Prof. Samwel Wangwe, alisisitiza kuwa kama usambazaji wa mafuta kutoka Russia utapungua, yanaweza kupanda duniani.

"Russia wanazalisha dhahabu kwa wingi wakiwa na changamoto, inawezekana dhahabu itapungua au bei itapanda, bei ya mafuta ikipanda tutaumia na bei ya dhahabu ikipanda itakuwa nafuu kwetu.

"Tunafanya biashara na Russia, na Ukraine kuna vitu tunauza kwenye soko lao, hivyo kwa vita hivi tuna changamoto ya kutafuta masoko mengine. Pia tuna biashara na Russia hasa wawekezaji wanaokuja Tanzania," alisema.

Prof. Wangwe alisema kwa sababu ni nchi mbili kubwa na Tanzania inafanya uhusiano nazo wanapoathirika moja kwa moja nchi nayo itaathirika.

"Mfumoko wa bei labda kupitia kwenye mafuta endapo yatapanda bei. Dunia inategemeana sehemu moja muhimu ikiumia lazima na sisi tutaipatapata," alisema.



UTAFITI WA MAENDELEO

TaCRI TANZANIA COFFEE RESEARCH INSTITUTE

# Mafanikio katika Utafiti wa Kahawa Tanzania

**TANGULIZI**

Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI) ilianzishwa mwaka 2000 kama kampuni ya dhamana yenye ukomo kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni (Kifungu. 212) na kuanza kazi kisheria tarehe mosi Septemba 2001 ikiwa na dhumuni kubwa la kuchangia ufufuaji wa tasnia ya kahawa kwa msisitizo mpya wa UTAFITI KWA MAENDELEO (R4D) unaoongozwa na wadau na kujibu mahitaji yao. Dira ya TaCRI ni kuchangia katika kuboresha tasnia ya kahawa Tanzania iwe na ustawi endelevu. Mwelekeo wake ni kuendeleza na kueneza teknolojia mwafaka ili kuinua tija na ubora wa kahawa ndani ya muundo mzuri wa sera. Matokeo tarajiwa ni kuongeza ushindani wa kahawa ya Tanzania katika soko la dunia na hatimaye kuongeza kipato, kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya wazalishaji wa kahawa.

Mwaka jana mwezi Septemba ilikuwa ni adhimisho la miaka ishirini ya TaCRI ila kwa sababu kadhawakadha ikiwemo tisho la ugonjwa wa UVIKO-19, hatukuadhimisha kwa mwembwe nyingi. Tumeandaa tu machapisho yatakayotoka hivi karibuni, yanayoelezea mafanikio ya taasisi katika kipindi hicho. Makala hii inaelezea kwa ufupi baadhi ya mafanikio hayo kiprogramu, changamoto zilizopo na mtazamo wetu wa siku za usoni.



*Jengo la utawala TaCRI Lyamungu na kilele cha Kibo kwa mbali*

# Uboreshaji wa Zao

Eneo hili linahusu uhaulishaji (breeding), tafiti za magonjwa (pathology) na vinasaba (biotechnology). Lengo ni kuendeleza, kuhakiki, kuzalisha na kusambaza aina za kahawa (Arabika na Robusta) zinazozaa sana, zenye ukinzani dhidi ya magonjwa, pia zenye punje kubwa na muonjo mzuri.

Programu ilirithi, kuhuisha na kuendeleza tafiti za nyuma zilizokuwa zikiendelea kwa kusuuasua na, kufikia mwaka 2006, tulishatoa aina mpya bora 10 za Arabika zilizo chotara zenye sifa zilizotajwa hapo juu. Aina hizo, ambazo ni kizazi cha kwanza ndefu, ni N39-1, N39-2, N39-3, N39-4, N39-5, N39-6, N39-7, KP423-1, KP423-2 na KP423-3. Tafiti mpya za TaCRI ziliibua aina nyingine tano, kizazi cha pili ndefu, zenye ukinzani thabiti kuliko zile za awali, nazo ni N39-8, N39-9, N39-10, N39-11 na N39-12. Hizi ziliidhinishwa rasmi mwaka 2013. Aina hizi zote, kwa vile ni chotara, huzalishwa kwa njia ya vikonyo.



*Aina za kahawa ya Arabika (kushoto) na Robusta (kulia) zinazozaa kwa wingi*

Hatukuishia hapo. Tulianzisha mpango wa kuendeleza aina fupi chotara na, mnamo mwaka 2015, aina 4 ziliidhinishwa, nazo ni TaCRI-1F, TaCRI-3F, TaCRI-4F na TaCRI-6F. Zaidi ya ukinzani wa CBD na kutu, aina hizi zina mwonjo bora kabisa, na huzaa kwa wingi zaidi. Tija kwa aina hizi ni mara 3-4 ya aina za jadi na mara 2-3 ya aina mpya ndefu. Kwa vile sasa tumekuwa na aina ndefu na fupi, ambazo mwonekano wake hauna mashaka, tumeendelea kutafiti uzalishaji wa mbegu chotara na tumefanikiwa. Tayari mbegu chotara zimekuwa mkombozi kwa uzalishaji wa miche kwani ni njia rahisi na ya haraka ya kuzalisha miche kwa wingi. Kwa sasa wastani wa tani 1.5 (Kg 1500) za mbegu chotara ambazo ni sawa na miche milioni sita (6) zinazalishwa.

Ugonjwa wa mnyauko fuzari (CWD) uliathiri kikubwa mibuni ya Robusta kule Kagera! Tangu ulipozuka mwaka 1997, ugonjwa huu umesababisha hasara ya tani 300 kila mwaka, zenye thamani inayozidi dola za kimarekani 200,000! TaCRI imetafiti na kutoa aina nne (4) za Robusta zenye ukinzani kwa ugonjwa huo hatari, nazo ni Maruku1, Maruku2, Bukoba1 na Muleba1. Aina hizi bora ambazo wakulima wanaziita "mkombozi", zimeongeza tija, faida na kuongeza kipato na riziki kwa wakulima. Aidha, aina zote hizi 23 zina hakimiliki (Plant Breeders Rights) na zinamilikiwa na TaCRI.

Utafiti wa kugundua aina zinazovumilia ukame ni changamoto ya hivi karibuni zaidi inayoletwa na mabadiliko ya tabia nchi. Utafiti huu unaendelea vizuri katika majaribio yaliyopo Wilaya za Rombo, Tarime, Kasulu na Mbozi. Takwimu za awali zinaonyesha kwamba kati ya aina tisa (9) zinazofanyiwa utafiti katika maeneo hayo, aina tatu (3) zimeonyesha uwezo wa kuvumilia ukame: N39-3, N39-10 na TaCRI 3F. Aina hizi ni miongoni mwa aina 19 za Arabika ambazo zimeidhinishwa rasmi na Wizara ya Kilimo. Utafiti kuhusu aina sita (6) zilizobaki unaendelea.



*Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya utafiti wa kahawa Tanzania (TaCRI), Dkt. Deusdedit Kilambo akiwa katika moja ya shamba la mfano Lyamungu - Kilimanjaro*



# UTAFITI WA MAENDELEO

## Tafiti za kilimo bora

Eneo hili linahusu rutuba ya udongo na lishe ya mimea, udhibiti wa visumbufu na makuzi ya mimea. Baada ya kutolewa aina mpya, mkazo sasa umeelekezwa katika kuibua mbinu mwafaka za ukuzaji zitakazoendana na aina hizo ili zikue kwa afya na kuzalisha kwa kadiri ya uwezo wake.

Utafiti wa kutambua maeneo ya upanuzi wa kilimo cha kahawa na rutuba ya udongo umekamilika katika mikoa 17. Mikoa hiyo ni: Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya na Songwe, (ambapo tulishirikishwa katika mradi wa Bodi ya Kahawa pamoja na Technoserve), Rukwa, Katavi, Kigoma, Kagera, Mara, Manyara, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Geita, Mwanza na Morogoro (ambapo tulifanya wenyewe). Taarifa za msingi za rutuba ya udongo katika mikoa hii zimewasilishwa katika halmashauri husika kwa matumizi ya maafisa ugani, pamoja na mapendekezo ya namna bora ya kutunza rutuba mashambani. Eneo jipya la upanuzi linakadiriwa kuwa ni zaidi ya hekta 15,000. TaCRI inawahamasisha wakulima kupima udongo wa mashamba yao ili kufahamu tabia zake, na inayo maabara ya kisasa kwa ajili hiyo.

Tulianzisha bustani ya viuatilifu asilia mwaka 2003 ikiwa na Utupa (Tephrosia vogelii) na Mwarobaini (Azadirachta indica). Kufikia 2007, bustani ilishapanuka kufikia hekta moja, ikiwa na aina 8 za mimea. Majaribio matatu ya kimaabara yalifanyika dhdi ya kimatira mwaka 2010 na ikaonekana kwamba kipimo cha chini cha gramu 1200 kwa lita kilikaribiana na rejea (Selecron). Tafiti za mitego ya ruhuka (CBB) zimeonyesha kuwa mchanganyiko wa 1:1 wa spiriti na maji, pamoja na vileo vya kienyeji kama mbege, dengelua, ulanzi na rubisi, vina uwezo mkubwa kama chambo cha kuwatega ruhuka. Teknolojia hii imeshaanza kuzoeleka miongoni mwa wakulima wadogo na wakubwa. Pia kiuatilifu cha Fipronil kilitafitiwa na kupendekezwa katika kudhibiti bungua weupe wa kahawa (WCSB) ambao wamekuwa ni tishio kwa tasnia ya kahawa katika maeneo mengi nchini.





*Kilimo mseto kilichopendekezwa cha kahawa na migomba (kushoto); majaribio ya kimaabara ya viuatilifu asilia (kulia)*

Kwa upande wa makuzi ya kahawa, tuliweza kubuni mtindo wa 3:1 wa kilimo-mseto cha kahawa na migomba kwa aina ndefu (mistari 3 ya kahawa ndani ya mistari 2 ya migomba) mwaka 2004; na 4:1 kwa aina fupi (mistari 4 ya kahawa ndani ya mistari 2 ya migomba) mwaka 2021. Mitindo hii imekubalika na wakulima kwa kuongeza tija. Mbinu tofauti za ukarabati wa mashamba zilijaribiwa, na ulengetaji, ukifuatiwa na upachikizaji ulionekana kuwa ni njia mwafaka zaidi, inayotoa fursa ya kubadili miti ya zamani kuwa mipya. Mambo haya, na mengine mengi yahusuyo kilimo bora cha kahawa, yameainishwa katika vitabu vya Kanuni Bora za Kilimo cha Kahawa ya Arabika (toleo la 1, 2011; na la pili, 2018), pitio la udhibiti husishi wa visumbufu vya kahawa (toleo la 1, 2011; na la pili, 2020) na Tabia za udongo wa kahawa (kipo kwa mchapishaji).

## Usambazaji Teknolojia na Mafunzo





*Mafunzo kwa wakulima (kushoto), uzalishaji wa miche (kulia)*

Mkazo katika eneo hili ni kutangaza na kusambaza teknolojia mwafaka za kahawa miongoni mwa wazalishaji ili kuongeza tija, kuinua ubora na kuongeza kipato. Hili hufanyika kwa kupitia mtandao wa vituo vidogo vilivyopo Lyamungu (Hai), Maruku (Bukoba), Mbimba (Mbozi), Ugano (Mbinga), Mwayaya (Buhigwe) na Nyamwaga (Tarime), maafisa ugani wa wilaya na kata, pamoja na wakulima wahamasishaji ambao tumewapatia mafunzo maalum.

Mafunzo ya kanuni bora za kilimo cha kahawa na uzalishaji miche yametolewa kwa wakulima wa kahawa 377,496. Zoezi hili linaendelea. Vipeperushi (leaflets) 185,707 juu ya kilimo bora cha kahawa vimeandaliwa na kusambazwa. Jumla ya maafisa ugani 10,865 wamepata mafunzo juu ya kanuni bora za kahawa. Wakulima wahamasishaji 3,849 wamepata mafunzo nchi nzima. Mafunzo zaidi yanatakiwa kuendelezwa kutokana na kuwepo kwa wagani wapya katika maeneo ya kahawa.

Bustani 400 zimeanzishwa nchi nzima katika kuzalisha miche chotara ya kahawa, toka mwaka 2002 Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali jumla ya miche 51,323,308 ya aina bora chotara ya kahawa imezalishwa (inayotosheleza Hekta 38,560) na kusambazwa kwa wakulima kwa ajili ya kuotesha mashambani, pia kuanzisha bustani mama.

**Uboreshaji wa maisha**

Wakulima waliofanya kazi shirika na TaCRI wamekuwa mifano ya kuigwa kwa kilimo bora, na mashamba yao kugeuka mashamba-mfano. Wengi kati ya wakulima wa aina hii huwa na vitabu vya wageni, kama ushahidi kuwa wanapata wageni mbalimbali toka ndani na nje ya vijiji vyao kujifunza kuhusu kahawa. Hili limewawezesha kuheshimika zaidi mbele ya jamii.

Wengi wa wakulima hawa mifano wameweza kuboresha makazi yao kwa kujenga nyumba za kisasa, wengine kununua vyombo vya usafiri na kuwekeza katika miradi mingine kama mifugo ya kisasa. Kwa upande wa kijamii, uwezo wa wakulima kuchangia katika miradi ya maendeleo ya jamii kupitia mapato yatokanayo na kahawa umeongezeka. Pia wengi wao wameweza kulipa ada za shule kwa watoto wao. Hivi ni vigezo vinavyopimika kwa kuonyesha maendeleo kifedha na kijamii. Wakulima waliopokea teknolojia za TaCRI ni wakulima wenye furaha!

**Kutambulika kitaifa, kikanda na kimataifa**

TaCRI imeimarisha mahusiano ya kitafiti ndani ya nchi kama vile Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Chuo Kikuu Nelson Mandela, Taasisi inayothibitisha ubora wa mbegu nchini (TOSCI), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Taasisi ya Utafiti inayoshughulikia viuatilifu (TPRI), kitengo kinachotoa hati miliki Wizara ya KILIMO (Plant Breeders Rights) ; na taasisi za kimataifa kama vile CIFC iliyopo Ureno, CIRAD na Nestle zilizopo Ufaransa na CABI iliyopo Uingereza. Kwa kipindi cha miaka 6 mfululizo toka mwaka 2010, Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa TaCRI amekuwa mmoja wa wanaounda Bodi ya Wakurugenzi ya "Association for Scientific Information on Coffee – ASIC" yenye makao makuu Geneva Uswisi.

TaCRI imeipaisha Tanzania hadi kuwa miongoni mwa nchi nane (8) duniani, na nchi tatu (3) Afrika zinazofanya vizuri sana katika utafiti wa kahawa. Tumetoa taarifa za Utafiti 57 kwenye makongamano (Conference); machapisho 19 kwenye majarida ya kimataifa (Peer reviewed journals) na "chapters") mbili kwenye vitabu. Mwaka 2011 Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ilizawadia TaCRI Jumla ya shilingi milioni 20, kwa tuzo ya kuwa taasisi bora nchini inayofanya tafiti na kutoa majawabu yanayokidhi mahitaji wa wadau. Mara mbili – 2006 na 2017, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) limetambua mchango wa TaCRI katika kutoa Mtafiti bora kitaifa. Taasisi imekuwa ikipata hati safi kutoka kwa wakaguzi wa fedha wa ndani na nje ya nchi.

**Changamoto**

Palipo na mafanikio hapakosi changamoto. Changamoto za kitafiti zinazoikabili TaCRI zinahusishwa na mabadiliko ya tabia nchi, kama vile mabadiliko ya tabia za wadudu waharibifu na magonjwa. Hii inatulazimu kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mwelekeo wa tafiti zetu ili kuendana na hali halisi. Kwa bahati, ufuatiliaji unaoendelea umedhihirisha kuwa ukinzani wa aina zetu kwa magonjwa ungali thabiti. Baadhi ya maeneo yaliyoibuka ni pamoja na kutafiti aina zinazohimili joto na ukame, aina zenye ukinzani dhidi ya wadudu waharibifu, teknolojia za makuzi zinazoendana na tabia nchi (climate-smart GAPs), nk.

Changamoto za kiugani ni pamoja na mahitaji ya miche bora kuzidi uwezo wa taasisi kuzizalisha na kuzisambaza.Tangu mwanzo wadau walisisitiza kuwa uzalishaji wa miche uwe ni jukumu la TaCRI pekee ili kulinda ubora. Katika mpango-mkakati wa tatu na wa nne, tulishauriwa tutafute wabia watakaofanya ugani na uzalishaji wa miche ili sisi, kwa idadi yatu ndogo ya watumishi 61 tu, tubaki na jukumu mama la utafiti, usambazaji teknolojia na uchechemuzi. Hata hivyo hili halijawezekana, kwa hiyo wadau bado wanaitegemea TaCRI kwa ugani na uzalishaji wa miche. Ili kukabiliana na changamoto hii, tumepanua mashamba yetu ya mbegu ili vikundi vya wakulima vipelekewe mbegu (na utaalam wa kuzisia) badala ya miche; na hii imeonekana kufanikiwa kwa kiasi fulani.

**Mwelekeo wa baadaye**

Mwakani tutapitia mpango-mkakati wa nne na kuandaa mpango-mkakati wa tano. Kama ilivyo kawaida yetu, maandalizi ya mpango-mkakati ni mchakato shirikishi ambapo wadau hupata fursa ya kuainisha changamoto zao na vipaumbele vyao ambavyo ndivyo vinakuwa msingi wa mpango-mkakati husika. Tafiti zote zinazohusika na mabadiliko ya tabia nchi zitaendelezwa, ikiwa ni pamoja na udhibiti husishi wa visumbufu (IPM), urutubishaji shirikishi wa ardhi (ISFM), idadi ya miti ya mibuni kwa eneo, idadi ya matawi yanayozaa kwa mti, nk. Lengo letu ni lile lile la kuibua na kuhamasisha teknolojia mwafaka zitakazoongeza tija na ubora, kuboresha riziki na kipato cha mkulima mmoja mmoja na pato la taifa kwa jumla; na kuimarisha nafasi ya Tanzania miongoni mwa wazalishaji wa kahawa duniani.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Corona bado ni tatizo, tuchukue hatua zaidi

**NI** wazi kwamba bado kuna haja ya wananchi kuchukua tahadhari zaidi ikiwamo kufuata mwongozo wa Wizara ya Afya na pia kwenda katika vituo vya kutolea chanjo ya UVIKO-19, ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa huo.

Umuhimu wa kuchukuliwa kwa hatua zaidi za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo unatokana na ukweli kwamba, tishio lake bado lipo nchini hasa kuzingatia takwimu zinazotolewa na serikali juzi.

Tunaamini kwamba Tanzania si kisiwa ambacho hakifikiki, bali ina mwingiliano mkubwa wa watu kutoka ndani na nje ya nchi, hivyo uwezekano wa usambazaji na maambukizi ya UVIKO-19 yapo.

Kwa kutambua madhara ya ugonjwa huo, serikali ilishatoa waraka wa kuwataka wananchi kuchukua tahadhari zote zikiwamo kunawa mikono kwa maji tiririka, kuvaa barakoa na pia kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Jambo lingine la msingi linalosisitizwa na serikali, ni wananchi kupata chanjo, lakini bado idadi ya wanaochanja haijaridhisha kutokana na kusuasua, hivyo nasi tunahimiza wananchi kuchukua tahadhari zote ili kuwa salama zaidi.

Juzi Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, alitoa taarifa kwa umma kuhuusu mwenendo wa ugonjwa wa UVIKO-19 nchini, ikionyesha kuwa watu 33,726 wamethibitika kukumbwa nao, huku 800 wakipoteza maisha kwa kipindi cha Machi, mwaka jana hadi Machi 4, mwaka huu.

Katika taarifa yake ya juzi, Dk. Sichalwe, anasema, idadi hiyo ni kati ya 471,965 sawa na asilimia 7.1 na waliopoteza maisha ni asilimia 2.5 na kwamba kuanzia Februari 5 hadi Machi 4, mwaka huu, kulikuwa na walioripotiwa kupata ugonjwa huo kati ya watu 31,090 waliopimwa na vifo vinane katika mikoa ya Mwanza (5), Dodoma (2) na Kagera (1).

Anasema, katika wagonjwa hao, visa 290 vilivyothibitika, mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa kuwa na wagonjwa 175 na kufafanua kwamba, kuanzia kipindi hicho cha Februari 5 hadi Machi 4, mwaka huu, wagonjwa wapya 136 walilazwa, kati yao 128 sawa na asilimia 94.1 hawakuchanja na mahututi walikuwa wanne.

Hali hii inadhihirisha kwamba ugonjwa huu bado ni tishio, hivyo sisi kama taifa bado tunalo jukumu kubwa la kuchukua hatua kujilinda na kulindana kama wataalamu wa afya wanavyoelekeza kuhusiana na hatua za kuchukua.

Wakati kukiwa na mwongozo, bado tunashuhudia baadhi ya watu katika maeneo mbalimbali ikiwamo Dar es Salaam, hawauzingatii, badala yake wanakusanyika na kujazana kwenye vyombo vya usafiri wa umma maeneo mengine mengi ya mikusanyiko kama sherehe, masomo, kwenye minada kwa kutaja baadhi. Suala la uvaaji wa barakoa ni kama limeachwa, kwani si jambo la ajabu kukuta ndani ya daladala abiria wamejazana kupita kiasi na hakuna hata mmoja ambaye amevaa barakoa.


Inawezekana kwa mazingira kama hayo, ndiyo maana Dar es Salaam inatajwa tena kwa mara ya pili kuwa kinara wa maambukizi ya ugonjwa huo, ingawa juhudi za kuhamasisha umma kujikinga na ugonjwa huo zimekuwa zikifanyika.

Kimsingi tunashauri, kila mmoja asipuuze maelekezo ya Wizara ya Afya, bali achukue hatua sahihi kuanzia kufuata mwongozo pamoja na kwenda katika vituo kwa ajili ya kupata chanjo, kwani Tanzania si kisiwa kisichofikika.

Tunashauri tahadhari hizo ziende sambamba na uchanjaji, kwani inaelezwa kuwa tangu chanjo ilizinduliwa Julai mwaka jana, hadi kufikia Machi 4, mwaka huu, zaidi ya watu milioni 2.6 tu ndio waliochanjwa. Kwa mujibu wa takwimu hizi, bado tunayo safari ndefu ya kufikia lengo la uchanjaji lililolewekwa na nchi yetu la asilimia 60 hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu. Ingawa kuchanja ni suala la hiyari, lakini linasababisha watu wanasuasua katika kuchanja.

Hakuna sababu ya kulazimisha watu kuchanja, lakini kwa baadhi ya majirani zetu kama Rwanda ambayo suala hilo ni lazima, wamefanikiwa kuchanja watu asilimia 75, hivyo tunashauri uhamasishaji uendelee kutiliwa mkazo tufikie malengo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili la nyavu haramu Victoria wengi tumo, sasa tujitathmini

Na Anthony Gervas, MWANZA

**SEKTA** ya uvuvi ni muhimu katika ustawi wa jamii, lakini ni 'pasua kichwa' kwa serikali, kutokana na kuwapo uvuvi haramu unaofanyika kila mara, kwa kutumia zana zilizozuiliwa na sheria.

Katika kurunzi langu leo namulika swali kwanini uvuvi haramu unaendelea kuwapo, wakati serikali inazipiga marufuku zana zile kutumika.

Najiuliza hilo litakoma lini? Ni kwa sababu kila mara utasikia, wamekamatwa watu kadhaa nyavu zile zimechomwa moto. Ni hali inayozidi kudumu na hatujui kitendawili hicho kitateguliwa lini.

Binafsi nauliza shida hiyo itakomeshwa lini na serikali? Au kitendawili hicho kitateguliwa lini, kimsingi unasababisha kuharibu mazalia ya samaki na kuua walio wadogo chini.

Swali la kujiuliza inakuwaje wavuvi haramu wanaendelea kusikika kila kukicha wakati wahusika wanatajwa walewale, watendaji wanaowajibika moja kwa moja kudhibiti hali hiyo iwe katika maeneo ya mialo au ziwani wanabaki kuwa wale wale? Ina maana waharibifu hawajulikani?

Kama wanajulikana, ninadadisi ina maana hakuna namna ya wahusika ama kukamatwa au kuchukuliwa hatua na kama wana maduka yanayohusiana na kashfa hizo, haifiki hatua hata ikibidi leseni za biashara hizo husika hazichukuliwi?

Wavuvi nao kama adhabu wanazopewa hazitoshi kuwarekebisha, nadhani hatua zaidi zinafaa inapobidi kwa mujibu wa mazingira yaliyoko au yanayotumika na wakati husika.

Nitoe mfano wa mahali niliko katika mkoa wa Mwanza na hata mingineyo inayozungukwa na Ziwa Victoria, utasikia kila mara maofisa wa serikali wamekamata wavuvi haramu, wakawanyang'anya nyavu hizo zikiwamo makokoro na kisha zinachomwa moto, lakini baada ya miezi kadhaa mambo ni yale yale kama vile hakujatokea kitu.

Ukiwafuatilia wananchi na wavuvi hao wanadai baadhi ya watendaji wa vijiji, kata na hata wilaya wasiokuwa waaminifu wanakuwa sehemu ya kujihusisha kwa namna mmoja au nyingine hata wakaruhusu mianya kufanyika, simulizi ya uvuvi haramu kuwa endelevu.

Nyavu zile hutumika nyakati za usiku tu kuvulia samaki, lakini maofisa uvuvi au watendaji unapoongea nao kama mwandishi wa habari utasikia wanasema umepungua kiasi kikubwa, wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha doria zao zinafanyika kuwasaka wahalifu wa aina hiyo.

Lakini, cha ajabu zikipita siku chache wavuvi wale wale wanaendelea kuvua wakitumia zana zilezile, hivi wanakuwa wanamdanganya nani maneno yao matamu? Kwanza samaki hawakui.

Nitoe mfano hai aina ya sangara. Pili, niseme wanaua mayai ya samaki wengi kutokana na kuharibu mazalia yao. Binafsi watendaji na wahusika wengine mnaosimamia na kudhibiti hayo acheni, nawasihi mfumbue macho.

Inafaa kuona mnachoma nyavu za mfano na moto wa kampeni uwashwe hasa na haifai hata kidogo kinyume na hapo. Kama kuna nyavu zimefichwa na wahusika, ili baadaye waendelee kuzitumia, kwa namna yoyote ile haitakuwa haki kwa umma.

Huwa tunasikia na kuona sana kutoka kwa mamlaka zetu, tukisikia "oooh samaki wamepungua sana ziwani, hivyo tufunge ziwa miezi kadhaa ili samaki wazaliane kwanza!" Kumbe chanzo ni makokolo, nyavu za buibui, timba na nyinginezo ambazo ni haramu kutumika.

Wahusika jamani, sisi wananchi tunafuatilia kubaini kitu gani kinaendelea. Dhambi hiyo itawatafuna siku moja, mayai ya samaki yanavuliwa na zana ya kumbakumba ambayo ni kokolo. Enyi ikiwa ni kweli mnajihusisha na dhambi hiyo, watendaji wa vijiji, kata, wilaya na wengine zote kwa nafasi tijitathmini.

Nyavu zinazoruhusiwa kuvulia zinatajwa kuwa za ukubwa wa nchi tano hadi sita, lakini wavuvi hao wenye zana haramu wanasemekana wana mbinu nyingi za kuficha nyavu hizo ikiwamo kuchimbia chini ya mchanga au ardhi ili wasitiwe nguvuni.

Tunapaswa kila mmoja wetu wananchi kufuatilia na kuchukua hatua tukishirikiana na serikali kuondoa changamoto, ikibidi iwekwe adhabu kali ya kifungo kwa wale wanaopuuza sheria na kusababisha kubakia kama kitendawili kisichoteguka kwa serikali siku zote.



Mke wa marehemu bilionea Erasto Msuya, Miriam Mrita (kushoto), akijadiliana jambo na mawakili wanaomtetea wakiongozwa na Wakili Peter Kibatala (wapili kushoto), katika kesi ya mauaji inayomkabili katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mahakama yakataa kupokea video ya tukio mauaji dada wa bilionea Msuya

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imekataa kupokea kielelezo cha 'video tape' yenye mahojiano kati ya Polisi na mke wa Bilionea Msuya, Miriam Mrita, akielezea tukio la mauaji ya dada wa bilionea huyo, Aneth Msuya.

Kukataliwa kwa kielelezo hicho kumetokana na kukiukwa kwa kifungu cha Sheria ya Makosa ya Jinai namba 246 (2).

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki baada ya kupitia hoja tano za pingamizi zilizowasilishwa na Wakili wa Utetezi Peter Kibatala na Wakili Nehemiah Mkoko. Akisoma uamuzi huo. Jaji Kakolaki alisema katika hoja tano zilizowasilishwa kupinga kielelezo hicho kupitia shahidi wa saba, Inspekta Aristides Kasigwa, mahakama imeona kuna hoja kubwa ya kujibu ambayo ni namba nne iliyowasilishwa na Wakili Kibatala akidai katika mahakama ya chini kifungu namba 246(2) cha CPA hakikuzingatiwa.

Jaji Kakolaki alisema katika hoja hizo inadaiwa video tape ambayo ni nyaraka ya kielektroniki haikuorodheshwa katika nyaraka zinazotakiwa kutumika kama ushahidi mahakamani na haikusomwa kwenye maelezo ya awali. Alisema hoja hiyo ilipingwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Genes Tesha, ambaye alidai upande wa mashtaka ulizingatia kifungu namba 246(2) na washtakiwa walielezwa upande wa mashtaka wanakusudia kutoa vielelezo halisi na video ilitajwa kwenye PH.

"Ni takwa la kisheria maelezo au nyaraka yoyote ya ushahidi inayokusudiwa kutolewa mahakamani ni lazima iorodheshwe na isomwe katika mahakama ya chini katika maelezo ya mashahidi.

"Kutosomwa kwa kielelezo kunaweza kusababisha kisipokewe mahakamani. Katika shauri hili kinachobishaniwa si maelezo ni kielelezo 'video tape' ambao ni ushahidi wa kielektroniki. "Kwa mujibu wa sheria, 'video tape' inatambulika kuwa ni nyaraka kama nyaraka zingine. Swali la kujiuliza ,je, nyaraka hiyo ilipaswa kusomwa na kuorodheshwa kuwa miongoni mwa vielelezo?

"Nakubaliana na Wakili Tesha kwamba maelezo ya shahidi yalisomwa katika maelezo ya mashahidi na kwenye PH. Kusomwa kwa maelezo ya shahidi hakukujitosheleza kujumuisha 'video' inayokusudiwa kutolewa kama kielelezo mahakamani," alisema Jaji.

Alisema yale yaliyosomwa yalikuwa maelezo lakini nyaraka hiyo ilipaswa kusomwa kwa kuwa hitaji hilo ni lazima kwa sababu linatoa uhakika na kumpa haki mshtakiwa ya usikilizwaji ulio sawa wakati wa kusikiliza shauri lake.

"Kutofanya hivyo mshtakiwa wa kwanza anakuwa anapokea ushahidi kwa kushtukiza, bila kumkosea heshima Tesha, mahakama haikubaliani na hoja yake. "Video tape ni nyaraka haiwezi kuchukuliwa kuwa ni kielelezo halisi, huu ni ushahidi wa kielektroniki, ushahidi halisi ni kama gari.

"Katika usikilizwaji wa awali kuna kielelezo kilitajwa CD video, je, CD video inamaanisha video tape? Hivi ni vitu viwili tofauti. CD inaweza kuzalishwa katika 'video tape' lakini 'video tape' haiwezi kuzalishwa katika CD video," alisema Jaji.

Alisema katika shauri hili mahakama haikuwekwa wazi CD video inamaanisha video tape na kwamba mahakama inapata wakati mgumu kusema kielelezo hicho kilisomwa wakati wa PH. "Baada ya kusema hayo mahakama inaona katika hoja hiyo kielelezo hakikusomwa hata katika PH, ni ukiukwaji wa kifungu namba 246(2) cha CPA. Kifungu namba 246(2) kinampa haki mshtakiwa wa kwanza kusikilizwa kwa usawa, mahakama hii inaona kuruhusu kupokelewa kielelezo hicho kutakuwa na madhara, kutamnyima haki mshtakiwa ya kujua ushahidi na kujipanga kujitetea.

"Ukizingatia shauri linalomkabili la mauaji ni kubwa. Nakubaliana na pingamizi namba nne, linatosha kumaliza mabishano ya hoja za pande zote mbili, sioni sababu ya kuzungumzia hoja zingine," alisema Jaji.

Alisema mahakama hiyo ilifikia uamuzi kielelezo hicho ambacho ni video tape yenye maelezo yaliyorekodiwa kwa mshtakiwa Miriam hakiwezi kupokelewa.

Awali Jaji Kakolaki alisema 'video tape' ilikuwa na maelezo ya mahojiano kati ya SP Latifa Mohammed na mshtakiwa Miriam , video ilichukuliwa Kituo cha Polisi Uwanja wa Ndege Agosti 8, 2016, Miriam alikuwa akielezea kuhusu tukio la mauaji ya Aneth na video hiyo ilichukuliwa na shahidi Inspekta Kasigwa ambaye aliomba mahakama ipokee kielelezo hicho. Wakili Kibatala na Nehemia walipinga kwa hoja tano lakini mahakama imetoa uamuzi kwa kuzingatia hoja namba nne na kuacha kuzungumzia hoja zingine nne.

Baada ya kumaliza kusomwa kwa uamuzi huo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tesha alidai hana shahidi mwingine hivyo mahakama iliahirisha kesi hiyo hadi kikao kingine cha mahakama. Katika kesi hiyo ya mauaji washtakiwa ni mke wa marehemu Bilionea Erasto Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyella.

Katika kesi ya msingi namba 103/2018 washtakiwa hao wanadaiwa kumuua kwa kukusudia Aneth Msuya, dada wa marehemu bilionea Erasto Msuya Mei 25, 2016 maeneo ya Kibada Kigamboni, Dar es Salaam.

## KESI YA SABAYA

# Shahidi aomba simu kizimbani

## ■Mwingine adai kushikiliwa TAKUKURU kwa wiki mbili

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa tatu wa utetezi, Watson Mwahomange, katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ameiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, kuiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kumpatia simu yake ili aitumie wakati akijitetea kizimbani.

Shahidi huyo ambaye ni mshtakiwa wa tatu katika kesi hiyo, alitoa maombi hayo jana mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi, Dk. Patricia Kisinda. Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

"Mheshimiwa hakimu; ninaiomba mahakama yako tukufu kuwaagiza TAKUKURU kuniletea simu yangu ili niitumie kama kielelezo wakati wa kujitetea," alidai.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofmed Mtenga, alidai kwamba mahakama haiwezi kutoa mwongozo labda awasiliane na TAKUKURU kwa kuwa kesi ni yake.

Wakili wa mshtakiwa wa kwanza na wa pili, Mosses Mahuna, alipinga ombi hilo kwa kuwa mahakama hiyo haiwezi kutoa maelekezo kwa kuwa kesi siyo ya madai, hivyo shahidi anatakiwa kwenda kutafuta vitu vyake mwenyewe na kuja kujitetea.

"Haiwezekani kutumia mwamvuli wa mahakama, anatakiwa kutafuta simu yake kwa kuwa kesi ni yake na aje kujitetea kwa kuwa mahakama haitambui kama ana simu," alidai.

Kutokana na pingamizi la Wakili Mahuna, shahidi huyo aliiomba mahakama kupinga hoja za mawakili hao kwa kuwa alikamatwa na yupo gerezani na TAKUKURU walichukua simu.

"Pia Mheshimiwa hakimu, Wakili Mahuna awali aliieleza mahakama kwamba tutakuwa na vielelezo vingi, hivyo ninaomba mahakama yako kutoa uamuzi na vielelezo vilivyotajwa mojawapo ni simu, ninaomba niitumie kujitetea," alidai huku Hakimu Kisinda akisema uamuzi kuhusu suala hilo utatolewa leo.

**WIKI 2 TAKUKURU**

Katika hatua nyingine, Shahidi wa Nne wa Utetezi, John Odemba, katika kesi hiyo jana alidai alishikiliwa na TAKUKURU kwa siku 14 bila kufikishwa mahakamani na kupewa nafasi ya kuzungumza na ndugu zake.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofmedy Mtenga, shahidi huyo alidai alizuiliwa katika Ofisi za TAKUKURU kwa muda wa siku 14 bila ya kufikishwa mahakamani na kupewa nafasi ya kuwasiliana na ndugu zake.

"Mheshimiwa hakimu nilishikiliwa kwa siku 14, nilipigwa na baridi kwenye sakafu kwa kipindi chote bila ya kupelekwa mahakamani na kupewa nafasi ya kuzungumza na ndugu zangu," alidai shahidi huyo.

Alidai kwamba kwa mujibu wa shahidi watano wa mashtaka, alimwona mshtakiwa huyo akiwa katika karakana ya Mroso na eneo la Benki ya CRDB Tawi la Kwa Murombo na alimkazia macho.

"Shahidi huyo wa tano alieleza mahakama alimwona mtu mwenye misuli kule aliyevaa buti za jeshi na fulana ya jeshi na hakusema kuwa ni mimi," alidai.

Aliendelea kudai kuwa hawezi kumleta mahakamani bwana jela kutoa ushahidi wa kuthibitisha kwamba maofisa wa TAKUKURU walitaka awapatie taarifa za Sabaya kwa kuwa siku hiyo alikuwapo wakati wa mazungumzo hayo lakini hahusiki kwenye kesi hiyo.

Akihojiwa na Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Jakopiyo Richard, shahidi huyo alikana kuonekana katika video za CCTV zikimwonyesha akiingia katika Benki ya CRDB Tawi la Kwa Murombo jijini Arusha.

Alidai kwamba hakwenda Kwa Murombo siku hiyo na hata benki hiyo, hivyo ushahidi uliotolewa na Mroso siyo wa kweli.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas, shahidi huyo alidai asingeweza kuwa mlinzi wa Sabaya kwa kuwa alikuwa Mkuu wa Wilaya na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na askari wote wapo chini yake.

Vilevile, alidai kwamba kwa mujibu wa shahidi wa 13 wa upande wa mashtaka, Ramadhani Juma, walipewa mgao wa fedha wakiwa Hoteli ya Tulia Lodge kutoka kwa Sabaya.

Shahidi huyo alikiri kuwasikia mashahidi wa 10 na 13 wa upande wa mashtaka, Mroso na Ramadhani, mtawalia, walidai mahakamani yeye alikuwa mlinzi wa Sabaya.

Shahidi wa Tano wa Utetezi, Jackson Macha (30) katika kesi hiyo alikana kuambatana na mfanyabiashara Mroso kwenda kuchukua fedha benki Sh. milioni 90.

Shahidi huyo ambaye ni mshtakiwa wa sita alidai kuwa Juni 14, 2021 akiwa nyumbani kwake, alifika Mjumbe wa Serikali ya Mtaa akiwa ameambatana na maofisa wa TAKUKURU wakimtaka kuondoka naye kwa kuwa walidai wanataka kufanya naye mahojiano.

"Kabla ya kuondoka walipekuwa nyumba yangu wakidai kwamba wanaangalia kama nina silaha.

"Walichukua simu zangu na ya mke wangu, pasipoti na cheti cha ndoa, lakini vitu vingine walivyochukua sikuviona," alidai.

Pia alidai hakuna ushahidi ulitolewa mahakamani kuthibitisha kuwa siku hiyo alikuwa kwenye eneo la hoteli hiyo wala kufanya mawasiliano na mtu aliyekuwa katika sehemu hiyo inayodaiwa kuundwa kwa genge la uhalifu.

"Mheshimiwa hakimu; mimi sikuwahi kwenda benki ya CRDB Tawi la Kwa Morombo nikiwa nimeambatana na Mroso na sikuwahi kufika huko na sipafahamu kabisa, nimekuja kupasikia hapa mahakamani wakati ushahidi ukitolewa.

"Mroso ni muongo, mimi sijawahi kufanya mawasilino na Sabaya na wenzake na pia taarifa ya mawasiliano ya Kampuni ya Vodacom imeonyesha kwamba sijawahi kuwasiliana na watu hao," alidai.

# Waziri akemea mila potofu umiliki ardhi kwa wanawake

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameitaka jamii kuondokana na dhana potofu kuwa bado kuna mila na desturi kandamizi katika umiliki wa ardhi kwa wanawake.

Ameitaka jamii kujadili changamoto zinazowakabili wanawake na vijana juu ya umiliki wa ardhi sambamba na jamii kuhamasishwa kuachana na mila na desturi potofu kuhusu umiliki wa ardhi kwa makundi hayo.

Dk. Mabula alisema Kifungu cha 3 (2) cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 ni mahsusi kinachotambua haki ya kila mwanamke kupata, kumiliki, kutumia au kuuza au kugawa ardhi kwa viwango na masharti sawasawa na wanaume.

Akizungumza wakati wa kufungua mjadala kuhusu wanawake na vijana kumiliki ardhi jijini Dodoma jana, Waziri Mabula alisema sheria yoyote ya kimila itakayowanyima wanawake, watoto au watu wenye ulemavu uhalali wa kumiliki mali, kutumia au kupata ardhi, basi itakuwa batili.

Alibainisha kuwa sheria za ardhi zimetoa kipaumbele kwa mwanamke kuwa na haki ya kumiliki ardhi isipokuwa mfumo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ndio unaomnyima haki.

''Sababu za kijinsia kiutamaduni kijamii na kiuchumi ndizo zinazomnyima haki mwanamke kwa kuwa hazitoi fursa rafiki kwa mwanamke," alisema Dk. Mabula.

Alitaka suala la elimu kupewa kipaumbele ili kuiwezesha jamii kuelewa haki za kisheria kwenye masuala ya umiliki wa ardhi na haki zingine zinazohusu vijana na wanawake pamoja na watoto.

Aliviasa vyombo vya habari kutumia nafasi yake vizuri kwa kuwa jicho la serikali katika kutoa elimu na ufahamu kwa wananchi kuachana na mtazamo hasi kuhusu wanawake na kuunga mkono juhudi za serikali kumyanyua mwanamke na kijana kiuchumi na taifa kwa ujumla.

Waziri Mabula aliitaka jamii kubadili fikra kuanzia katika ngazi ya familia kwa kuwa hatua hiyo itasaidia suala la mila na desturi kandamizi kuondoka kwa kuwa kizazi kitakuwa kimeona ubaya wa kile wazee waliokuwa wakikithamini.

Pia aliwataka wazazi kuwa na tabia ya kutambua vipaji vya watoto wao wangali wadogo na kuhakikisha wanawaendeleza kupitia vipaji hivyo ili waweze kuwa wataalamu huko mbeleni katika masuala mbalimbali.

Naye Mwakilishi wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), Nuru Pipino, alsema wanawake na vijana wamekwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali katika masuala ya ardhi ikiwamo kuota mizizi kwa mila na desturi potofu kwa wanawake na vijana pamoja na uelewa mdogo kwa mwanamke kumiliki ardhi.

''Kumekuwa na changamoto mbalimbali kuhusiana na masuala ya ardhi kwa wanawake na vijana kama vile mila na desturi potofu sambamba na maeneo yanyochukuliwa na serikali kupewa kwa watu wenye fedha na kuachana makundi ya vijana na ardhi hiyo kukodishwa tena kwa makundi hayo," alisema Pipino.




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula akifungua mjadala kuhusu umiliki ardhi ya kilimo kwa wanawake na vijana, jijini Dodoma jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

## Nchi zinazoongea Kifaransa zasherehekea lugha

**Na Beatrice Shayo**

BALOZI za nchi 13 zinazowakilishwa nchini Tanzania ambazo zinaongea lugha ya Kifaransa zinaadhimisha sherehe za umuhimu wa lugha hiyo ambayo inawaunganisha pamoja na kuchochea amani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, alisema nchini Tanzania balozi 13 zitaadhimisha siku ya kimataifa ya Francophonie ambayo ilianza jana hadi 26 mwaka huu.

"Tutasherehekea lugha ya Kifaransa na Francophonie kwa lengo la kukuza lugha hiyo, anuwai ya lugha na kitamaduni ambayo inatufanya tuendelee kushikamana kwa amani na upendo," alisema Balozi.

Alisema kuanzishwa kwa Francophonie ni kutumia lugha ya Kifaransa kama njia ya kukuza mshikamano na maendeleo na kuleta jumuiya mbalimbali kuwa pamoja.

Balozi alisema asilimia 59 ya wanaozungumza Kifaransa wanaishi Afrika na idadi hiyo inatajwa kuongezeka hadi asilimi 80 ifikapo 2050.

Alisema nchini Tanzania idadi inaongezeka ya wanafunzi na wataalamu wanaojifunza Kifaransa na inaonyesha dhamira kubwa ya kushiriki katika ushirikiano wa kiuchumi na kisiasa Afrika.

"Takribani Watanzania milioni 1.5 wanajua Kifaransa ambayo ni lugha ya kigeni isipokuwa Kiingereza inayotolewa kama chaguo katika mtaala wa shule katika Ulaya ni lugha ya pili kujifunza zaidi," alisema.

Balozi alisema ili kusherehekea lugha ya Francophonie wataonyesha tamasha, maonyesho ya sanaa, filamu, onyesho la mitindo na tamaduni mbalimbali.

Naye Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo nchini, Jean Pierre, alisema Kifaransa kinapaswa kufundishwa nchini kwa sababu lugha ya Kiswahili inaleta amani, upendo kupitia lugha ya Kifaransa.

Alisema nchini kwake wanafunzi wanasoma somo la Kifaransa na kwamba ni muhimu kujifunza lugha hiyo ambayo ni muhimu kwa kuwa baadhi ya nchi inatoa kipaumbele katika kuitumia.

**Balozi alisema asilimia 59 ya wanaozungumza Kifaransa wanaishi Afrika na idadi hiyo inatajwa kuongezeka hadi asilimi 80 ifikapo 2050.**

# Mabilioni ya EU kukuza mnyororo wa mazao

**Na Romana Mallya**

MRADI wa Agri-Connect wa Euro milioni 100 (sawa na Sh. bilioni 277) unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) ambao kati ya fedha hizo, Euro milioni 12 zimezinduliwa kusaidia ukuzaji wa mnyororo wa thamani kwa mazao ya kahawa, chai na kilimo cha bustani Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakati wa uzinduzi wa mfuko maalum wa AgriFI kwa Tanzania wenye kiasi cha Euro milioni 12 aliomba kati ya fedha hizo, Euro milioni nne zielekezwe Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa.

"Ninawaomba EU muuangalie mradi wa chai wa hekta 6,000 uliopo Kilolo ambao kwa muda mrefu umekufa licha ya kuwa na miundombinu, Agri-Connect kupitia fedha hizi za AgriFI Euro milioni nne ninaomba zielekezwe kufufua mradi wa Kilolo ili wakulima nao wanufaike," aliomba.

Akichanganua fedha hizo, Bashe alisema kati ya Euro milioni 100, Euro milioni 48 zitatumika kuboresha barabara za vijijini katika Nyanda za Juu Kusini kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Alisema kwa muda mrefu kumekuwa na tatizo la miundombinu ambalo husababisha wakulima wa chai kila mwaka hupoteza tani milioni nne ya majani ya chai ambayo hayafiki sokoni.

"Uamuzi wa kuwekeza katika barabara ni muhimu, ninawashukuru EU kwa kushirikiana na serikali katika mradi wa kuanzisha mnada wa chai Tanzania ambao ulikuwa uzinduliwe Desemba mwaka jana ila haukufanyika lakini utafanyika wakati wowote mwaka huu," alisema.

Balozi wa EU nchini, Manfredo Fanti, aliahidi umoja huo utaendelea kushirikiana na Tanzania katika eneo hilo la sekta ya kilimo na kufafanua kuwa mradi wa Euro milioni 12 utawanufaisha watu 4,000.

Balozi Fanti alisema Agri-Connect inawaunganisha wakulima na masoko kupitia uwekezaji katika ukarabati wa miundombinu vijijini.

Programu ya Agri-Connect (2019-2025) inasaidia miradi kadhaa ambayo inachangia katika ukuaji shirikishi na endelevu wa minyororo ya thamani wa mazao tajwa juu kwa ajili ya kuboresha mapato na kufungua uwezo wa minyororo ya thamani ili kuboresha maisha ya jamii za vijijini.

Programu hii kwa ujumla imelenga kuboresha maisha ya wakulima wadogo 150,000 katika Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania na Zanzibar.

"Itachangia katika ukuaji shirikishi wa uchumi, maendeleo na uwekezaji katika sekta binafsi, utengenezaji wa ajira na kuboreshwa kwa usalama wa chakula na lishe.

# ACT sasa yaishauri jamii kutambua wanawake

**Na Christina Mwakangale,** MKURANGA

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimesema ni wakati sasa wa kulitambua kundi kubwa la wanawake, kwa kuondoa vikwazo na kuendeleza mapambano yao.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Dorothy Semu, aliyasema hayo wilayani Mkuranga mkoani Pwani, wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Wanawake Duniani, yaliyoandaliwa na chama.

Alisema wanawake walioko kwenye siasa na nyadhifa tofauti watoe ushirikiano na kusaidia kuondoa unyanyasaji, ubaguzi, ukandamizaji dhidi yao.

"Sisi tuliopo kwenye siasa tuhakikishe vyama vyetu vinagusa matamanio, matarajio, malengo, maslahi yao. Tuungane nao kwa kuwashirikisha, kupaza sauti zao kusukuma ajenda zao ambazo ni ustawi wa jamii kwa ujumla," alisema Semu na kuongeza:

Kwa miongo takribani miwili harakati za wanawake zilipamba moto kufikia kupata nafasi kadhaa kwenye nafasi za uongozi, takwimu zinaonyesha pamoja na jitihada hizo bado kuna wanawake tunawaacha nyuma."

Alisema siku hiyo ni muhimu kwa wanawake kutokana na kwamba inatoa fursa ya kuwaimarisha nchini, ikiwamo nafasi za uongozi na uwakilishi.

Aidha, kwa niaba ya chama hicho, Semu alikabidhi zawadi kwenye wodi ya kinamama wajawazito katika hospitali ya Wilaya Mkuranga, zikiwamo pampazi za watoto, taulo za kujistiri wanawake, maji ya kunywa pamoja na sabuni ikiwa ni kusherehekea siku hiyo.

Katibu wa chama hicho Mkoa wa Pwani, Mohamed Mtambo, akizungumza baada ya kukabidhiwa zawadi hizo, alisema, anawashukuru wanawake wa chama hicho kwa kuwakumbuka kinamama wa Mkuranga.

"Ni faraja kwangu na heshima pia maadhimisho ya Siku wa Wanawake Duniani kitaifa kufanyika hapa, tuendelee kuunga mkono juhudi za wanawake kwa kuwa wanasaidia kuendeleza gurumu la maendeleo kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Mtambo ambaye alikuwa mgombea wa ubunge wa Jimbo la Mkuranga, alibainisha kwamba, chama kitaendelea kushirikiana na jamii ili kuhakikisha inajikwamua kiuchumi.

# JKT yafunguka madai ya uwapo rushwa, upendeleo

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limesema limewaondoa hofu wananchi kuhusu taarifa za uwapo wa rushwa na upendeleo katika mchakato wa kuandikishwa kwa vijana wa kujiunga na jeshi hilo kwa mujibu wa sheria na kujitolea.

Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, ndiye aliyetoa ufafanuzi kuhusiana na taarifa hizo, na kuwaondolea hofu Watanzania kuwa ndani ya jeshi hakuna rushwa.

Meja Jenerali Mabele alisema kwamba hakuna rushwa ili vijana kujiunga kwenye jeshi hilo, na kwamba kinachozingatiwa ni vigezo vikiwamo umri na afya.

Jenerali Mabele aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam, kwenye kipindi cha Dakika 45, kinachorushwa na kituo cha televisheni cha ITV.

Alisema jamii iondoe dhana kwamba nafasi za kujiunga na jeshi hilo zina upendeleo akisema iwapo wanaofanya hivyo wanakiuka kiapo walichoapa.

"Hakuna rushwa katika kupata fursa JKT, nafasi hizi haziuzwi. Hicho kitu hakipo, ila wapo wanaofanya utapeli kwamba wanatoa nafasi kwa vigezo visivyo vyetu kama jeshi. Tumekula kiapo lazima uwepo uadilifu," alisema Meja Jenerali Mabele.

"Ila kama ipo rushwa, ambayo inaweza kutendeka kwa watu wawili namna ya kupatikana ushahidi wa hilo hukuchukua muda kubaini."

Aliongeza kwamba, mafunzo yanayotolewa kwenye kambi tofauti kwa miezi minne kwa vijana walioteuliwa kujiunga hulenga kuwafunza uzalendo, uadilifu, ujasiri, kujitegemea, uhodari na uaminifu.

Pia alisema JKT imekuwa ikifanya shughuli tofauti za uzalishaji ikiwamo kushona share za jeshi, na kwamba matarajio ya miaka miwili ama mitatu ijayo ni kuongeza uzalishaji wa mazao na kujilisha wenyewe.

"Mwaka 2024/25 tutaanza kujilisha. Kwa sasa tunaendeleza kazi kama kauli mbiu ya serikali yetu. Tangu niingie kwenye nafasi hii ilikuwa kipindi cha UVIKO-19, nashukuru Mungu vijana wote waliojiunga kwenye kambi tofauti hakuna aliyepa maambukizi na kambi zilienedelea kama kawaida," alisema Meja Jenerali Mabele.




Ofisa Ustawi wa Jamii wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Jastin Chambo (wanne kulia), akipokea msaada wa viti mwendo na dawa za matibabu kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Ubora wa Huduma wa Benki ya Afrika, Anna-Roberta Mango, vilivyotolewa na benki hiyo, hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mulamula ahimiza usawa kijinsia kwenye ajira

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amewata waajiri kuzingatia usawa wa kijinsia wakati wanapoajiri.

Amesema uwapo wa wafanyakazi wengi wanawake katika kampuni kunaongeza thamani pamoja na mafanikio katika kampuni husika.

Alitoa rai hiyo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa kikao cha Jukwaa la maofisa watendaji wakuu wa kampuni (CEOrt) wakiadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Balozi Mulamula alisema sekta binafsi nchini inatambua umuhimu wa wanawake katika utendaji lakini endapo watahitaji kufika mbali na kupata mafanikio wanapatwa kuzingatia usawa wa kijinsia wakati wa kuajiri.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametengeneza mazingira mazuri ya uwekezeji kwa kampuni za ndani na za nje.

Na inafahamika kwamba sekta binafsi ndiyo wenye mchango mkubwa katika kuinua uchumi wa nchi. Lakini wanapaswa kuzingatia usawa," alisema Balozi Mulamula.

Balozi Mulamula alisema kampuni nyingi duniani zimefanikiwa kwa kuajiri idadi kubwa ya wanawake, hivyo aliwataka CEOrt kuhakikisha nao wanaongeza idadi ya wanawake katika ajira.

"Kampuni ili zinaendelea kwa sababu ya kuajiri wanawake, leo (juzi) ni Siku ya Wanawake Duniani, hivyo Rais Samia Suluhu Hassan amenituma kumwakilisha kwenye mkutano huu nizungumze na maofisa watendaji wakuu wa kampuni na kuwapa salamu zake," alisema Balozi Mulamula.

Mwenyekiti wa Ceort, Sanjay Rughan, alisema: "Tumemsikia waziri, tunaahidi tutaleta usawawa kijinsia katika kampuni zetu kwa sababu itaongeza uwezo, faida. Tumeona jitihada zinazofanywa na Rais Samia katika sekta binafsi."

Alisema CEOrt kwa muda mrefu imekuwa mtetezi mkubwa wa utofauti na ushirikishwaji kwamba uwakilishi wa wanawake katika uanchama umeendelea kukua.

Rughan alisema kumekuwa na ongezeko la asilimia 86 kwa viongozi wa kike ndani ya CEOrt, kwamba imedhamiria na kuweka malengo dhabiti kwa mpango wake katika uongozi bora.

Rughan alisema: "CEO kupitia program mbalimbali inatarajia kuongeza ushiriki wa wanawake kutoka asilimia 25 hadi 40 ifikapo mwaka 2025.

# Sababu za kushuka mfumuko wa bei

**Na Romana Mallya**

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imesema mfumuko wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia Februari, mwaka huu umepungua hadi asilimia 3.7 kutoka asilimia 4.0 ulivyokuwa mwaka unaoishia Januari.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Takwimu za Kijamii, Ruth Minja, alisema mfumuko wa bei kwa taifa unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi.

Alisema kupungua kwa mfumuko wa bei kwa mwaka unaoishia mwaka unaoishia Februari kumechangiwa na kupungua kwa mfumuko wa bei wa baadhi ya bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula kwa kipindi hicho ikilinganishwa na Januari.

"Bidhaa za vyakula zilizoonyesha kupungua kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Februari, ikilinganishwa na mwaka ulioishia Januari ni pamoja na: matunda (kutoka asilimia 9.5 hadi asilimia 5.2); mbogamboga (kutoka asilimia 5.0 hadi asilimia 3.7); kunde (kutoka asilimia 7.1 hadi asilimia 2.6).

"Njegere (kutoka asilimia 6.8 hadi asilimia 4.2); siagi (kutoka asilimia 6.6 hadi asilimia 6.5); tambi (kutoka asilimia 4.2 hadi asilimia 3.9) na bidhaa za ngano za kutoka (kutoka asilimia 8.4 hadi asilimia 5.8)."

Alisema baadhi ya bidhaa zisizo za chakula zilizoonyesha kupungua kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Februari ikilinganishwa na ule wa Januari ni pamoja na: nguo za watoto (kutoka asilimia 3.5 hadi asilimia 2.9) na mkaa (kutoka asilimia 6.4 hadi asilimia 6.1).

Nyingine ni magodoro (kutoka asilimia 7.3 hadi asilimia 6.2) na huduma za vyakula kwenye migahawa kutoka asilimia 2.7 hadi asilimia 1.9.

"Kwa ujumla mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia Febuari umepungua hadi asilimia 6.1 kutoka asilimia 6.3 kwa mwaka ulioishia Januari mwaka huu," alisema.

Alisema mfumuko wa bei ambao haujumuishi bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwezi Februari nao umepundua kwa asilimia 2.7 kutoka asilimia 3.1 ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Januari.

Alisema Uganda mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Februari umeongezeka hadi asilimia 3.2 kutoka asilimia 2.7 kwa mwaka ulioishia mwezi Januari na Kenya umepungua hadi asilimia 5.08 kutoka asilimia 5.39.




Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la AMREF Health Africa Tanzania, Dk. Florence Temu (katikati), akisikiliza maelezo kuhusu mkaa mbadala unavyofanya kazi kutoka kwa mmoja wa wanufaika wa mradi wa Taka Mali na Afya, Tausi Hassan (kushoto), unaotekelezwa na shirika hilo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake watakiwa utayari wa kujifunza

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE nchini wametakiwa kuwa na utayari wa kujifunza mambo mapya yatakayowawezesha kufikia malengo yao kiuchumi.

Wito huo umetolewa na Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT). Akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwenye ofisi za makao makuu ya kituo hicho jijini Dar es Salaam, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi SAGCOT Beng'i Issa, mbali ya kuwapongea wanawake wote duniani kwa kuazimisha siku hiyo aliwataka kuwa na utayari wa kujifunza ili waweze kupambana na changamoto mbalimbali zinazowakabili kufikia malengo waliyojiwekea.

"Ninapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wanawake wote kwa kuazimisha siku hii na ninachukua nafasi hii kuwahimiza kuwa na utayari wa kujifunza ili muweze kukabiliana na changamoto zinazowakabili na kufikia malengo kiuchumi," alisema Beng'i Issa.

Alisema kielelezo cha taifa kuongozwa na Rais shupavu na jasiri kama Mama Samia Suluhu Hassan kinaonyesha ni kwa jinsi gani taifa limepiga hatua na kutambua mchango wa wanawake kwenye jamii na kuwataka wanawake wengine kuziangazia changamoto wanazokutana nazo kama fursa ya kupiga hatua kwenye maisha.

"Ni imani yangu kwamba uwepo wa rahisi wetu mahiri kutaleta msukumo chanya kwa wanawake wengine wengi zaidi kutambua kuwa wanaweza na ni suala la kujiamini na kujitambua na kuwa tayari kujifunza," alisema Bi, Beng'i Issa.

Aliongeza: "Mtaji mkubwa wa mafanikio ni kujituma na kuwa na mahusiano mazuri kazini na adui mkubwa wa kufikia malengo ni uvivu, hivyo ni vitu ninavyotaka niwasihi wanawake wote kuvizingatia ili kuwa na mafanikio."

Kwa upande wa Mkurugenzi wa kampuni ya BIG FISH inayojishughulisha na ufugaji wa samaki, Zena Mndeme, aliwataka wanawake kutobweteka na shughuli moja bali wajishughulishe na shughuli zingine za uzalishaji ili waweze kuongeza kipato.

"Wengi wetu tunajisahau na kubweteka na kazi pasipo kujishughulisha na ujasiriamali, hii inawanyima waanawake wengi fursa ya kujiongezea kipato, sasa nitoe ushauri kwa wanawake wenzangu kuchangamkia fursa hizi adhimu za kujikwamua kiuchumi," alisema Mndeme.

Alisisitiza: "Mwanamke makini ni yule anayejitambua na hasiyetegemezi kwa mwanaume na mwenye kujitambua, kujikubali na kujifunza kufikia malengo kiuchumi."

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya AKM Glitters, Elizabeth Swai, aliwataka wanawake nchini kuwa na uthubutu kwa kuzichangamkia fursa mbalimbali zilizoko ili waweze kuinua maisha yao kiuchumi.

"Kumekuwa na hofu na wasiwasi mkubwa kwa wanawake wengi wanapotaka kufanya shughuli za ujasiriamali, hivyo basi natoa rai kwa wanawake wote nchini kutokata tamaa na tuwe na uthubutu wa kujaribu kufanya jambo," alisema Swai.

Aidha, Mkurugennzi Mtendaji wa SA GCOT, Geoffrey Kirenga, aliwapongeza wanawake wote kwa kuazimisha siku hiyo na kuwataka kuchangamkia fursa zilizoko kwenye sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ili waweze kujiongezea kipato.

"Miongoni mwa sekta zilizotoa fursa kubwa kwa wanawake wengi kuweza kushiriki moja kwa moja ni sekta ya kilimo na ufugaji, hii inatoa mwanga kwa wanawake wengine wengi kuona manufaa yaliyoko kwenye sekta hizi ili waweze kunufaika nazo moja kwa moja," alisema.

## Wanafunzi wanolewa kujiandaa na maisha

**Na Gwamaka Alipipi**

WANAFUNZI zaidi ya 500 wa Shule ya Sekondari Kurasini jijini Dar es Salaam wamepewa elimu ya kujiandaa na maisha ya kazi kwa miaka ya baadaye.

Elimu hiyo ilitolewa na kampuni ya kuuza mafuta ya magari iitwayo Vivo Energy, lengo kuu likiwa ni kuwapatia elimu ya vitendo wanafunzi wa sekondari, pindi watakapomaliza masomo yao wawe tayari kufanya kazi kwa ufanisi.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo hayo, Meneja Masoko na Mawasiliano wa Vivo Energy, Grace Kijo, alisema: "Leo tumekuja kutoka elimu ya kujiandaa na kazi kwa maisha ya baadaye kwa wanafunzi wa sekondari. Elimu tunayowapa ni ya vitendo na siyo nadharia kwa sababu elimu ni bora kuliko kitu chochote".

Kijo alisema elimu ya vitendo inamjenga mwanafunzi kuwa imara zaidi kuliko elimu ya nadharia anayopewa darasani.

"Wanafunzi tunawaandaa katika maisha yao. Idadi kubwa ya watu waliopo vijijini wanakosa elimu hii. Hivyo tutajitahidi zaidi kuwafikia watu wote waliopo mjini na vijijini. Hii ni mara yetu ya kwanza kufanya tukio hili hapa nchini," alisema Kijo.

Alisema Vivo Energy ni kampuni ya kuuza mafuta ya magari, kwamba ipo katika nchi 23 barani Afrika, hapa nchini ina vituo 38.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kurasini, Marcelino Fussi, alisema: "Tunajisikia furaha kutembelewa na kampuni ya Vivo Energy ambayo imekuja kuwapatia elimu ya kujiandaa na kazi kwa maisha ya baadaye wanafunzi wetu. Elimu hii ni muhimu kwa sababu wanafunzi wengi hawana ujuzi wala uelewa wa masuala ya kazi."

Hivyo, alizikaribisha kampuni zingine kufika shuleni hapo kutoa elimu mbalimbali kwa wanafunzi wa shule hiyo.

Mmoja wa wanafunzi katika shule hilo ambaye ni Dada Mkuu, Songe Edward alisema: "Kwa leo mimi ni binti badaye nitakuwa mama. Nimefurahi kupata elimu ya masuala ya kazi kutoka Kampuni ya Vivo Energy".

Aliongeza: "Wanafunzi wa kike hapa shuleni tunapata matatizo mengi ambayo tunahitaji msaada ikiwamo sehemu za kuhifadhia taulo za kike. Pamoja na mahitahi ambayo mtoto wa kike lazima ayapate akiwa shuleni. Hivyo ninaomba kampuni na taasisi zingine zije kutupatia msaada."



Ukurasa 14

**Kutimia miaka mitatu ya Corona na mbinu kukabili mgeni Omicron**



Ukurasa 13

**SIKU YA FIGO DUNIANI**

...Darasa la wataalamu Muhimbili kuhusu mzizi, vita vya kutibu figo



Ukurasa 12

**SIKU YA FIGO DUNIANI**

**Serikali inavyojipanga tiba figo iwe kitaifa bajeti ijayo**

AFYA

DODOSO ZA 'BAIBAI' SIKU YA WANAWAKE

# Mama wa watoto 19 asimulia makuu yanayosibu ulezi wake

• Kila mwaka amejifungua, wote wenye afya njema

**Na Mwandishi Wetu**



Mama Mboze Munga Chiro, akilea watoto wake. **PICHA: MTANDAO**

JE, unaweza kutamani kuwalea watoto zaidi ya 10 kwa wakati mmoja? Sasa mwanamke mwenye umri miaka 49 kutoka eneo la Kilifi, pwani ya Kenya amebahatika kupata watoto 19.

Mboze Munga Chiro, ni mama wa watoto 10 wa kiume na tisa wa kike. Mtoto wake wa kwanza ana miaka 32 na kitinda mimba miaka miwili.

Amekuwa akijaliwa kupata mtoto kila mwaka, akibahatika wote wana afya nzuri, ingawa alimpoteza mmoja wa kike.

Keao alikotoka, mama huyo - Mboze ni mwana pekee katika familia, lakini kutokana na maisha magumu ya ufukara aliyoyapitia nyumbani, aliamua kuolewa mapema kabla hajakomaa vilivyo. Yalikuwa matumaini yake kwamba, kuolewa huenda kungemkomboa dhidi ya magumu na kupatikana unafuu walau wa yaliyo ya msingi kama vile chakula, nguo na upendo, vitu ambavyo hakuvipata nyumbani alikotoka.

Anasema, aliingia katika ndoa alipokuwa na umri wa miaka 17 akiishi na mpenzi wake huyo na haikuchukua muda mrefu, ndoa hiyo ya kwanza ikaharibika.

Hapo akajaliwa mtoto wake wa kwanza wa kiume na kila mwaka akawa anajifungua mtoto hadi akawa na watoto watano.

Lakini maisha hayakuwa rahisi ya kuwalea watoto hao, kwani mume wake alikuwa akifanya kazi ya vibarua kwenye majengo, yeye naye akiajiriwa kupalilia na kulima mashamba ya watu.

Mboze anasimulia watoto wake watatu wa kwanza alisaidiwa na wakunga wa nyumbani, hasa pale alipokuwa anajifungua, lakini alipoendelea kujaaliwa watoto zaidi majirani walianza kumsema na kumcheka kwa kuwa anajifungua kila mwaka. Hapo ilimbidi aanze kujifungua bila usaidizi wa mtu yeyote.

"Nimezaa mpaka nimemaliza hata huyu wa mwisho nimejifungua peke yangu," anasema Mboze na kwamba aliwapa majina watoto wake wawili pekee na wengine walipewa majina na mumewe.

Baadhi yao walipewa majina ya watu waliomtembelea baada ya kujifungua na wapo wengine waliopewa majina tofauti ya watu tajika duniani kama Bruno, Bruce Lee na Sadaam.

Ingawa mwanamke huyo anasema anawafahamu watoto wake wote kwa majina yao, huwa ni vigumu kwake kukumbuka wanavyofuatana kwa kuzaliwa.

"Mimi hata sijui huyu ni mtoto wa ngapi. Mara nyingi lazima nifikirie au nihesabu mmoja baada ya mwingine, ndio nijue ni mtoto wangu wa ngapi.Lakini, nawapenda watoto wangu wote sawasawa," anasema.

Mboze alipokuwa amejifungua mtoto wa 18, alirudi kwa daktari kutafuta usaidizi, lakini alipofanyiwa uchunguzi wa kimatibabu alikutwa na ujauzito mwingine. Hapo akawaomba madaktari wamsaidie kupanga uzazi.Baada ya kumpima, anakumbuka kauli ya madatakari akiwanukuu walimwambia: "Mama una mayai matano".

Hapo ndipo akaamua kufunga kizazi chake na kusema hatamani mtoto wake hata mmoja awe na kizazi kama chake.

**VURUGU YA CHAKULA**

Mtoto wake wa 13 Munga aliyeko darasa la saba, anaeleza magumu anayokutana nayo katika kuishi ndani ya familia kubwa, kwamba kuna changamoto aina yake hata kupata kiamsha kinywa, huwa ni vigumu.

Anasimulia kuwa hata chakula wakati mwingine hawapati na iwapo kitapatikana angalau mara moja kwa siku, mara nyingi huwa hakitoshi.

"Mara nyingi kuna vurugu kwa sababu ya chakula hakitoshi, kwa sababu wengine hawashibi wanataka chakula cha wengine," anasema mama huyo.

"Kama leo tumeamka hatukupata kiamsha kinywa tukienda shule na hivi sasa ni saa saba na pia hatuna hata maji ya kunywa.'

"Nina Imani kuwa, siku moja moja tutapata chakula na baada ya masomo yangu natamani kuwa wakili ili niwajengee wazazi wangu nyumba ya kuishi, "anasema.

Anaeleza dhamira yake siku moja awe wakili , ili aweze kuisaidia familia yake.

"Sitaki kuwa na watoto wengi, natamani tu watoto watano kwa sababu ninachokipitia ni hali ngumu" anasema.

Mtoto mwingine wa 11 kuzaliwa, anaeleza kufurahia maisha ya kuzaliwa kwenye familia kubwa, kwani anashuhudia amani licha ya anachokitaja 'changamoto za hapa na pale.' Anaendelea: "Mimi sipendezewi na haya mazingira, ndio maana najituma niende shule,nije niisaidie familia yangu."

Mtoto huyo anasema wazazi wake wamemfundisha kutokuwa na wivu na watu, kujiepusha na ugomvi na kuwapenda watu wengine.

**• Kwa mujibu wa BBC**

AFYA

## SIKU YA FIGO DUNIANI
## MAPAMBANO YALIVYO UWANJANI

# Serikali inavyojipanga tiba figo iwe kitaifa bajeti ijayo

• Vifaa tiba vyaja kila mkoa kunufaika

**Na Yasmine Protace**



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu. **PICHA: MTANDAO**

MARADHI ya figo yana kawaida ya kuwatesa wanaougua, hasa wanapofikia hatua ya kuanza kuisafisha figo.

Dhana 'kuwatesa' inabeba tafsiri pana ya matumizi makubwa ya fedha na yanayoendana nayo. Cha kujiuliza, iwapo mgonjwa asiye na bima ya afya atahitajika kuhudumia hitaji hilo au mwenye kipato kidogo analimudu vipi hilo?

Hivi karibuni serikali imetangaza inatumia fedha wastani wa shilingi bilioni 29, kufanya huduma za kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo 1000 nchini kwa mwaka.

**KAZI YA FIGO**

Figo inatajwa kuwa miongoni mwa viungo muhimu mwilini mwa binadamu. Kukosekana kwake, kunasababisha magonjwa na hata umauti kwa mwanadamu. Figo limejengwa kwa viungo vingi, pia kazi nyingi.

Kazi kuu mbili ni, kutoa uchafu unaoathiri mwili na kuweka usawa wa maji (fluids), madini na kemikali.


Figo inatoa mkojo, uchafu wenye sumu na maji zaidi kutoka mwilini. Mkojo unaotengenezwa katika figo hupitia mrija uitwao" ureta na unateremka hadi kwenye kibofu, kisha kutokea kupitia mrija wa 'urethra'. Kazi muhimu za figo zimeelezwa hapa chini.

Kutoa uchafu; Kusafisha damu kwa kutoa uchafu ni kazi muhimu sana ya figo. Vyakula tunavyokula huwa na protini. Protini ni muhimu kwa kukua na kurekebisha mwili. Mkusanyiko wa uchafu huo ni sumu mwilini. Figo inachuja damu na uchafu hatari (wa sumu) na hutolewa katika mkojo.

Kutoa maji mengi; kazi yake ya pili muhimu ni kulinganisha 'majimaji' kwa njia ya mkojo na kubakiza kiwango muhimu cha maji mwilini, ikibakisha kiwango kamili kinachohitajika na kukiwapo ziada ya maji, mwili unavimba.

Kusawazisha madini na kemikali; figo inasawazisha madini na kemikali kama sodium, potassium, hydrogen, calcium, phosphorus, magnesium na bicarbonate na ikiacha kiwango kamili cha maji mwilini. Kubadilika kiwango cha sodium, kunaathiri fahamu na kubadilika potassium, ikidhuru mapigo ya moyo na kufanya kazi kwa mishipa. Kuweka kiwango sawa cha calcium na phosphorus ni muhimu kwa afya ya mifupa na meno.

Kuchunga shinikizo la damu; figo hutoa homoni mbalimbali (rennin, angiotensin, aldosterone , prostaglandin ....) na kusawazisha maji na chumvi mwilini, kufanya kazi muhimu kulinda msukumo wa moyo. Usumbufu wa kutoa hormoni na kusawazisha chumvi na maji kwa mwenye ugonjwa wa figo, humuongezea msukumo wa damu.







Inazalishaji chembe za damu: Inafanya kazi muhimu katika kutoa chembe za damu nyekundu (RBC).Figo likishindwa hilo, huangukia kuwapo chembe hemoglobin kidogo na kuugua anemia.

Kuendeleza mifupa yenye afya; Figo inabadilisha Vitamin D mwilini katika hali yake ya kutumika, ikinyonya madini calcium kutoka kwenye chakula, kuwezesha kukua mifupa na meno na kuiweka katika afya.

Figo ikishindwa kufanya kazi, kwa upungufu wa Vitamin D, ukuaji mifupa unasuasua. Hivyo ni ishara ya kwanza kwa watoto walio na shida ya figo.

**UPANDIKIZAJI FIGO**

Anasema kuna jumla ya wagonjwa 93 nchini wameweza kupandikizwa figo, ila shida iko katika idadi ndogo ya walio tayari kutoa figo ya kupandikiza.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, upandikizaji figo unagharimu kiasi cha shilingi milioni 30, huku dawa zake zikiuzwa kwa bei ya wastani wa shilingi milioni mbili.

Dk. Linda anasema mpango mkakati wa huduma za figo wa mwaka 2021/22 sasa ni kuimarisha huduma ya kinga, ikiendana na kufanyika utafiti wa figo.

**MIKAKATI SERIKALINI**

Mdhibiti Ubora kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Joseph Kitukulu anasema: "Serikali inatumia zaidi ya shilingi bilioni 29.484 kwa mwaka, kufanya huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa 1000."

Katukulu anasema kupitia Bohari Kuu MSD, itaokoa zaidi ya shilingi bilioni 13, hivyo kuboresha upatikanaji huduma zinazoambatana na hizo.

Mratibu wa Figo kutoka Wizara ya Afya, Dk. Linda Ezekiel, anasema: "Kusafisha figo ni gharama,ambapo mgonjwa mmoja hutumia zaidi ya shilingi milioni 40 kusafisha figo."

Dk. Linda anafafanua, katika kukabiliana na matumizi makubwa ya usafishaji figo, MSD imeagiza mashine za kusafisha damu kutoka kwa watengenezaji, ili kuwezesha upatikanaji huduma hiyo kwa gharama nafuu na rahisi kwa wagonjwa wa figo hapa nchini.

Dk. Linda anasema, wagonjwa wa figo kitaifa wanakabiliwa na gharama kubwa ya huduma hizo na serikali kupitia MSD tayari imeshaagiza mashine 171 za kusafisha damu na mashine za kuchakata maji 11.

Utaratibu uliopo ni kwamba, mashine hizo zinapelekwa moja kwa moja kwenye hospitali zilizoandaliwa kutoa huduma hiyo na Dk. Linda anafafanua katika kipindi cha mwaka mmoja wa utawala uliopo madarakani, serikali imewekeza zaidi ya shilingi bilioni moja kuhudumia usafishaji upatikane katika hospitali zote nchini.

Dk. Linda anataja takwimu za kitaifa kwamba, takribani wagonjwa 1000 wana tatizo la figo nchini anaendelea: " Kati ya wagonjwa hao 5800 na 8400 wanaohitaji huduma ya kusafisha damu, 2750 tu wanapata huduma hiyo."

Anasema kwa sasa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) inahudumia wagonjwa wanaosafishwa figo kati ya 200 hadi 300; Bugando ya Mwanza wako 150; Aga Khan 25; na Hospitali ya Regency ina wagonjwa 40, zote ni za jijini Dar es Salaam.

Dk. Linda anaeleza katika Hospitali ya Mloganzila ya jijini Dar es Salaam, nayo inahudumia jumla ya wagonjwa 25 kwa siku; Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya ina wagonjwa 25; Hospitali ya Rufani Lindi wagonjwa saba; KCMC ya Kilimanjaro kila siku inahudumia wagonjwa 40

Anasema, hadi sasa mikakati ya kiserikali ni kuhakikisha hospitali zote nchini zinatoa huduma ya kusafisha figo. Hadi sasa kuna jumla ya vituo 45 kitaifa vya kusafisha figo. Dk. Linda anataja katika kipindi cha mwaka 2015, miaka saba iliyopita kulikuwapo watu zaidi ya milioni 1.5 duniani waliopoteza maisha kutokana na ugonjwa wa figo na waliokosa huduma za kusafisha figo walikuwa milioni 7.1 kwa mwaka huo.

Hivi karibuni kuna hospitali 10 zimepatiwa vifaa vya kusafishia figo, zote katika ngazi ya rufani, akizitaja kuwa ni: Amana, Temeke, Mwananyamala (zote za Dar es Salaam), SekoToure (Mwanza), Morogoro, Dodoma, Mawenzi, Chato, Songea na Mbeya.

"Juni 23 /2022 nchi nzima itakuwa inatoa huduma za kusafisha damu," anaeleza.

•Soma zaidi Uk 13

AFYA

## SIKU YA FIGO DUNIANI

# ...Darasa la wataalamu Muhimbili kuhusu mzizi, vita vya kutibu figo

**Na Mary Geofrey**

SIKU ya Figo Duniani huadhimishwa kila Alhamisi ya wiki ya pili ya mwezi Machi, kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii kujikinga na kujitokeza kupata matibabu ya ugonjwa huu.

Nchini, maadhimisho hayo huadhimishwa na Wizara ya Afya kwa ngazi ya kitaifa na mkoa, kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii, kuufahamu ugonjwa huo na namna ya kujikinga nao.

Kaulimbiu ya Siku ya Figo inasema 'afya ya figo kwa wote, tuondoe pengo la uelewa wa afya ya figo, kufikia huduma bora ya figo'. Wataalamu wa afya wanawasilisha takwimu kuwa asilimia 6.7 ya kundi hilo wanaugua magonjwa ya figo, huku wakikosa uelewa wake kiundani.

### SABABU ZA UGONJWA

Bingwa wa tiba za watoto, Dk. Jackline Shoo, anasema sababu za ugonjwa huo ni mengine yasiyoambukiza kama vile kisukari, shinikizo la damu na ugonjwa wa ndani wa viungo.

Anataja magonjwa ya papo kwa papo, yanayompata mtu ndani ya muda mfupi kutokana na hali kama kifafa cha mimba, kung'atwa na nyoka au nyuki, mshituko, malaria au ajali.

Aidha, anataja ugonjwa sugu unaotokana na mengine kama kisukari, shinikizo la damu, saratani, kuziba mkojo, homa ya ini na matumizi holela ya dawa za kuondoa maumivu.

Dk. Jackline, anasema kutumia mitishamba kunachangia kuenea ugonjwa huo unaoathiri wengi nchini, sambamba na magonjwa ya kurithi kama lupasi; ugonjwa unaonyemelea mfumo wa kinga.

### FIGO KWA WATOTO

Daktari huyo anasema, watoto wadogo wanapata magonjwa sugu na takwimu za hospitalini hapo, zinataja katika kila watoto 50 wanaofika kliniki moja, yupo mmoja mwenye shida ya figo.

Pia, anaeleza sababu za kuwapo ugonjwa sugu wa figo kwa watoto wadogo, ni ama kwa kuzaliwa wakiwa na shida ya kuziba njia ya mkojo kunakosababisha vibofu kujaa na sababu nyingine ni mtu anazaliwa akiwa na malengelenge, hitilafu na kuziba njia ya mkojo.

Dk. Jackline anaeleza pale mtoto mdogo anapoharisha na kutapika muda mrefu, hatari yake ni kupatwa na ugonjwa wa figo. Anaendelea: "Elimu kwa jamii inahitajika mtoto akitapika na kuharisha awahishwe hospitali kupata matibabu haraka ili kumuepusha na tatizo hili."

Bingwa wa Magonjwa ya Ndani ya Mwili na Figo, Dk. Mazhar Amirali, anasema katika maradhi sugu ya figo, mgonjwa anaweza kuishi nayo kwa miaka mitano pasipo kuhisi aina yoyote ya kasoro, ilhali ameathirika kwa zaidi ya asilimia 90.

"Ndiyo sababu tunahamasisha jamii kujitokeza kupima afya mara kwa mara ili kuepuka kuwa katika hatari kubwa ya tatizo," anaeleza.




Mkazi wa Tanga, Merry Michael akiwaeleza waandishi wa habari afya ya mtoto wake, Othniel Kimaro, baada kupandikizwa figo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), aliyochangiwa na mama yake, Merry. Huduma hiyo ilianza mwaka 2017. **PICHA ZOTE: MNH**

### GHARAMA IKOJE?

Dk. Amirali anasema, wastani wa kusafisha figo kwa mwezi inamgharimu mgonjwa kati ya Sh. Milioni nne hadi tano na kupandikiza hutumia zaidi ya Sh. milioni 20.

"Mtaona gharama za matibabu zilivyokuwa kubwa, ndio sababu tunaendelea kuhamasisha jamii kujikinga au kuepuka kupata maambukizi," anasisitiza Dk. Amirali.

Anasema, zipo dalili za wagonjwa sugu kama vile kukojoa damu au mawe madogo; kukosa usingizi usiku, kutapika, kichefuchefu na mwili kuchoka pasipo sababu.

"Kikubwa unaweza kuwa na ugonjwa wa figo usijue, ndio sababu tunawaambia wajitokeze kupima magonjwa ya shinikizo la damu na mkojo, kuangalia kama kuna protini," anasema.

Katika maadhimisho ambayo kilele chake ni leo, Chama Cha Madaktari wa Figo nchini wanatumia siku hiyo kutoa elimu kwa jamii, wakiwa na ujumbe: "Tunatumia siku katika maeneo yote nchini kutoa elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa huu waufahamu, wajitokeze kutibiwa na namna ya kuepuka."



Bingwa wa Tiba Magonjwa ya Figo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Jacqueline Shoo.

> **Mtaona gharama za matibabu zilivyokuwa kubwa, ndio sababu tunaendelea kuhamasisha jamii kujikinga au kuepuka kupata maambukizi.**

### NINI KIFANYIKE?

Daktari Bingwa wa Magonjwaya Figo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Onesmo Kisanga, anasema utafiti unaonyesha duniani kote ugonjwa wa figo upo kwa asilimia 10.

"Kuna utafiti uliofanyika kwa njia ya kaya, ambao ulionyesha kuwa asilimia 6.7 wana ugonjwa wa figo nchini, kwa sababu ya kukosa uelewa na ndio sababu kauli mbiu yetu inatutaka tutoe elimu kwa jamii," anaeleza.

Dk. Kisanga anaeleza madhimisho ya leo wanaelimisha watumishi wa afya kuhusu uelewa wa ugonjwa wa figo na elimu ya jamii inahitajika hasa vijijini, kwa sababu hawana hamasa ya elimu inayohusu figo, hata uelewa wake sahihi.

"Vijijini kuna ambao wanaamini dawa za miti shamba zinazuia magonjwa ya figo, lakini sisi wataalamu tunafahamu matumizi ya dawa za mitishamba ambazo hazijapimwa zinasababisha ugonjwa huu," anasema.

### WATAALAMU WALIVYO

Dk. Kisanga anasema kitaifa wako madaktari bingwa wa figo 31, kati yao wapo kinamama 15 waliosambazwa katika hospitali mbalimbali nchini, akifafanua idadi ya madaktari ilianza kuongezeka mwaka 2000.

Anasema huduma za matibabu ya figo zinatolewa kote nchini katika hospitali za mikoa na kanda, ambako unapimwa figo, mashine za kuzisafisha na huduma nyinginezo kukabili ugonjwa huo.

Daktari huyo anafafanua tayari kuna vyuo vya tiba nchini vinavyotibu figo; madaktari na wauguzi. Pia, madaktari bingwa wanaendelea kuelimisha watunga sera na sheria, waje na vinavyosaidia huduma za figo nchini.

### KUUZUIA UGONJWA

Dk. Kisanga anaelimisha kuwa haimgharimu mtu kupima afya yake ili ajikinge na ugonjwa huo, kwa sababu wanapima mkojo na shinikizo la damu na hatua nyingine ni kuendelea kuelimisha jamii kuachana na matumizi ya dawa bila ushauri wa daktari, akitoa angalizo la matumizi ya dawa zisizo rasmi.

Pia, Dk. Kisanga anasema hivi sasa idadi ya wagonjwa inaongezeka, sababu mojawapo ni watu kutobadili mtindo wa maisha kama vile kula, watu hawapimi afya zao, akieleza sababu kubwa ya kuwapo ugonjwa huo ni matatizo ya uzazi, malaria, pia saratani.

Hapo anasema, kwa wiki wanasafisha damu wagonjwa 300, huku kwa mwezi wanapokea wagonjwa wapya 25 wanaofanyiwa huduma hiyo na waliamua kuanzisha Chama cha Madaktari Bingwa wa Figo ili watoe elimu endelevu kwenye huduma za afya, wakishirikiana na serikali.

AFYA

# Kutimia miaka mitatu ya Corona na mbinu kukabili mgeni Omicron

• Kenya rasmi mzalishaji wa vidonge vinavyotibu



Sehemu ya vidonge kutibu Covid 19, vilivyoanza kuzalishwa nchini Kenya. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

JANGA la vifo vitokanavyo na maradhi Covid 19, sasa linachangia vifo kwa kiwango cha kutisha, hesabu iliyoko duniani leo ni wastani wa watu milioni sita, hata kutoa salamu kimataifa hali sio ya masihara.

Ikiwa na umri wa miaka mitatu sasa, leo hii iko katika hatua ziadi kwa kirusi cha Omricon, kinaleta balaa kimataifa na idadi ya wanaofariki, wengi wamo katika orodha ya wasiopata chanjo.

Tikki Pang, ni Profesa katika Chuo Kikuu cha Singapore, anasema idadi ya vifo duniani inaripotiwa zaidi kwa watu ambao bado hawajapokea chanjo dhidi ya virusi hivyo.

Anaeleza ilimchukua miezi saba kurekodi watu milioni moja wa kwanza waliokufa baada ya ugonjwa wa Covid-19 kutangazwa kuwa janga la dunia mwaka juzi na miezi minne baadae, watu wengine milioni moja walipoteza maisha.

Pia, anasema tangu wakati huo, kuna wengi wamekuwa wakipoteza maisha kila baada ya miezi mitatu na kufikisha takwimu hizo zinazoshabiana na vifo vya wastani milioni sita

Idadi hiyo inatajwa huenda ikawa kubwa zaidi kutokana na kutokuwepo takwimu kamili za watu waliokufa katika sehemu nyingine duniani.

Tathmini iliyofanywa na timu ya wataalamu katika jarida la kimataifa la The Economist, wanakadiria uhalisia wao kuwa idadi ya vifo vilivyotokana na ugonjwa wa Covid-19 ni kati ya milioni 14 na 23.

Hapo ndipo kunatajwa picha halisi ya hatari ilivyo, akiwataka watu wasipuuze masharti ya kudhibiti kusambaa kwa corona kwa kutovaa barakoa na mengineyo husika.

> “Ilianza na mgonjwa aliye na dalili nyepesi. Alisema alikuwa na uchovu mwingi kwa siku mbili na alikuwa anaumwa mwili na kichwa. Hakuwa akikohoa, hakupoteza harufu au ladha.

Chuo kikuu cha John Hopkins, Marekani katika utafiti wake kinasema, visiwa vya Pacific, ambavyo kwa zaidi ya miaka miwili vilikuwa vimenusurika na maambukizo ya virusi vya corona, navyo sasa vinaandamwa na vifo vinavyotokana na aina mpya ya kirusi cha Omicron.

Kadhalika, kisiwa cha kibiashara cha Hong Kong, pia kinashuhudia ongezeko la vifo kutokana na ugonjwa wa Covid-19, huku kisiwa chenye idadi ya watu milioni 7.5, sasa kinapima wakazi wake mara tatu kwa mwezi, katika hali ya kujaribu kudhibiti kuenea janga corona.

Maeneo mengine ya Ulaya Mashariki, Poland, Hungary, Romania na mataifa mengine ya Ulaya Mashariki, kunatajwa kushuhudia wakimbizi milioni moja wanaokimbia vita nchini Ukraine, huku maeneo hayo ya nchi imekuwa na idadi ndogo ya watu waliopokea chanjo ya Covid-19.

Marekani, nako licha ya utajiri wake na upatikanaji rahisi wa chanjo dhidi ya Covid, idadi ya vifo vinavyotokana na ugonjwa katika taifa hilo inakaribia watu milioni moja.

**OMICRON ILIKOTOKEA**

Inatajwa kwamba inasambaa kupitia matone ya mate yatokayo mdomoni au puani mwa mtu aliyeambukizwa na mara nyingine aina hiyo ya ugonjwa haina dalili, hata kuifanya igundulike baada ya muda.

Lakini, wengi walioambukizwa wanakumbwa na usumbufu wa kuishiwa nguvu kufikia hata kulazwa na hatari kubwa kiafya, jambo linaloibua tena umuhimu wa kujua na kutumia njia za kujikinga.

“Matumizi ya maski, kukaa mbali na mtu mwingine na chanjo bado ndizo hatua muhimu,” anaeleza mtaalamu.

Ripoti kutoka kwa madaktari waliomtibu mgonjwa wa kwanza nchini Afrika Kusini, zinaonyesha mabadiliko muhimu kwenye dalili, huku mtaalamu Dk. Angelique Coetzee, anasema watu hao mara nyingi hukumbwa na uchovu, uchungu kwenye misuli kuwashwa koo, joto na kukabiliwa na kikohozi kikavu.

“Ilianza na mgonjwa aliye na dalili nyepesi. Alisema alikuwa na uchovu mwingi kwa siku mbili na alikuwa anaumwa mwili na kichwa. Hakuwa akikohoa, hakupoteza harufu au ladha,” anafafanua tabibu huyo.

Mtaalamu Dk. Fonseca, ana maelezo yenye ushauri wa mtu kuwa makini, akifafanua: “Habari zinazokuja kutoka Afrika Kusini za dalili nyepesi zinatupa matumaini, lakini tunahitaji bado kuchunguza zaidi.’

Eneo lingine la ufafanuzi ni kwamba kunahitajika uelewa wa kina kuhusu omicron na tabia zake kwa watu wenye umri tofauti na kati ya makundi yao, ili wajiweke sawa kuikabili.

**KILICHOKO AFRIKA KUSINI**

Ngazi ya juu ya maambukizi ya virusi Corona nchini Afrika Kusini imeonyesha mlipuko uliochochewa na aina mpya ya virusi mwishoni mwa mwaka, mkoa wa Gauteng, ndiko kumeripotiwa maambukizi mapya 3,582 kwa siku moja.

Hata hivyo, kiwango hicho ni kidogo ikilinganishwa na hali ilivyokuwa wiki moja kabla, kuwapo mikasa 7,488 iliyoripotiwa katika muda kama huo, kwa mujibu wa tathmini iliyotolewa na asasi ya NICD, Desemba mwaka jana.

Maeneo yaliyoathirika zaidi yanajumuisha mkoa wa mashariki wa Kwazulu Natal, hasa katika eneo lake la pwani.

**UGUNDUZI KENYA**

Kenya imepata ridhaa mwezi huu kutengeneza vidonge vya kumeza kupambana na maradhi Covid 19, hadi sasa kampuni 27 za Afrika na Asia zimeshateuliwa kutengeneza dawa hiyo itakayogawanywa kwa mataifa 105 masikini.

Shirika la Universal, lililopo nje kidogo ya jiji la Nairobi, litavitengeneza vidonge hivyo, vikimilikiwa na kampuni ya Strides Pharma Science ya India, watengenezaji wa dawa za kupambana na makali ya Ukimwi na inatambuliwa rasmi na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Dk. Willis Akhwale ni Mwenyekiti wa jopo kazi la kupambana na Covid 19 nchini Kenya, akibariki uzalishaji huo anasema, mkataba ulifikiwa kati ya kampuni ya utafiti na bidhaa na ya utabibu ya Merck iliyo na kibali kamili.

Pia, makubaliano yanajumuisha shirika la Medicines Patent Pool linaloungwa mkono na Umoja wa Mataifa kuzishusha bei za dawa kwa mataifa masikini.

Shirika hilo liliteua kampuni 27 katika mataifa ya Bangladesh, China, Misri, Jordan, India, Indonesia, Pakistan, Afrika Kusini, Korea Kusini, Vietnam na Kenya.

Molnupiravir ni dawa inayoweza kuua virusi na iliundwa mahsusi kwa mafua. Ni dawa ya kunywa na inaweza kutumiwa nyumbani kutibu Covid 9 isiyokuwa kali.

Wataalamu wa dawa hiyo wanashauri inapaswa kutumiwa katika hatua za mwanzo za maambukizi, kuepusha madhara zaidi. Hata hivyo, wagonjwa wenye umri chini ya miaka 18 hawapaswi kutumia Molnupiravir, kwani inaweza kuathiri ukuaji wa mifupa yao.

Waziri wa Afya, Mutahi Kagwe, ana ufafanuzi wa mkataba kwamba shirika la MPP litashusha bei za dawa kwa mataifa masikini, kampuni tano zitajikita kwenye kuandaa mali ghafi na 13 zitaitengeneza malighafi na dawa.

Pia, kampuni tisa zilizosalia zitakamilisha mchakato wa kuiunda dawa na kampuni ya Kenya iliyoteuliwa ya Universal Corporation itahusika na hatua ya mwisho za kuandaa dawa.





# Bashungwa ataka taratibu zifuatwe utekelezaji mradi DADP

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amezitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinafuata utaratibu uliopangwa katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Wilaya (DADPs).

Bashungwa aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na Wataalamu wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Kilimo na Wadau kutoka Taasisi ya Kendeleza kilimo Afrika (AGRA).

Alisema mpango huo utasaidia kuongeza uzalishaji na kuongeza mapato, lakini utasaidia kuwa na malengo katika kufanya shughuli za uzalishaji wenye kuleta tija.

Waziri Bashungwa alisema, ili kuwezesha halmashuari kufanya kazi za kilimo katika kuongeza uchumi wananchi aliagiza mamlaka hizo kutumia ipasavyo maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji.

Aliagiza Maofisa Ugani kusimamia mpango huo ili kuhakikisha wananchi wanafanya shughuli zao za uzalishaji na wananufaika nazo.

"Huu mpango umetupa mwongozo wataalamu, mradi huu ni wa awamu ya pili sasa nitoe wito kwa viongozi wenzangu ukianza kutekelezwa tukausimamie ili wananchi tunaoenda kuwasimamia wanakuwa na maslahi nao," alisema.

Alibainisha mpango utaanza kutekelezwa katika mikoa 12 na halmashauri 30 Kagera (Muleba, Misenyi na Biharamulo), Kigoma (Kasulu, Kibondo na Kakonko), Katavi (Tanganyika, Mpimbwe na Nsimbo), Rukwa (Kalambo, Nkasi, Sumbawanga DC), Ruvuma (Songea DC, Madaba na Mbinga DC).

Pia Njombe (Wanging'ombe, Ludewa), Iringa (Mufindi, Kilolo), Manyara (Babati, Hanang' na Kiteto), Arusha (Meru, Karatu na Arusha DC), Kilimanjaro (Hai, Siha na Rombo), Simiyu (Maswa) na Tanga (Kilindi).



Mwanamke mfanyabiashara wa nyanya, akipanga bidhaa yake, wakati akisubiri wateja katika Soko la Sabasaba, jijini Dodoma jana. Kipimo cha nyanya kwenye ndoo ya ujazo wa lita tano huuzwa kwa 3,000/- hadi 5,000/. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mtendaji kortini tuhuma za ubadhirifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Chemba, imemfikisha mahakamani Kaimu Mtendaji wa Kata ya Latra, Eva Masawe kwa tuhuma za ubadhirifu wa mali ya umma na kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 3.8.

Kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba mbili ya mwaka 2022 ilisomwa jana na Mwendesha Mashtaka wa taasisi hiyo, Leonard Haule mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Chemba, Ester Mwakalinga.

Akitoa taarifa ya kesi hiyo, Mwendesha Mashtaka huyo, alidai mtuhumiwa huyo anadaiwa kutenda kosa hilo Machi hadi Aprili mwaka 2020.

"Baada ya TAKUKURU kufanya uchunguzi tumebaini kosa hili na tumechukua hatua za awali za kisheria za kumfikisha mahakamani mtuhumiwa huyo kwa ajili ya taratibu nyingine za kisheria kuendelea," aliiambia mahakama hiyo.

Alidai ubadhirifu huo umefanywa kupitia ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine za kukusanyia ushuru (POS) ambazo zinapaswa kuwasilishwa katika halmashauri kwa mujibu wa taratibu zilizopangwa na serikali, lakini hakufanya hivyo.

Mhtakiwa baada ya kupandishwa kizimbani alisomewa shtaka lake na kukana, hivyo aliachiwa kwa dhamana.

Kesi hiyo itatajwa tena Machi 21, mwaka huu.

# Wanawake TCDC wataka watoto wenye mahitaji vituoni kusaidiwa

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), wamewataka wadau na taasisi mbalimbali kuwasaidia watoto wenye uhitaji walioko kwenye vituo vya kuwalea ili kupata mahitaji ya msingi kama wengine.

Ofisa Utawala wa TCDC, Joyce Kato, aliyasema hayo juzi walipotoa msaada kwenye kituo cha kulea watoto yatima cha Kijiji cha Matumaini jijini hapo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Alisema kuna umuhimu wa kutoa misaada mbalimbali ili watoto wasikose mahitaji yao ya msingi.

"Tumechagua kijiji cha Matumaini kwa kuwa sisi kila tunaposhiriki maadhimisho tunachagua kituo cha kwenda kutoa msaada, mwaka jana tulienda Buigiri lakini sasa hivi tumechagua Matumaini kwa sababu hawa wana mahitaji sana," alisema.

Alisema nia ya dhati ya TCDC ni kuwasaidia watoto kwa kuwa wamekuwa wakipata matatizo mbalimbali.

"Wito wetu kwa taasisi zingine tujitoe tukipata uwezo wa kusaidia kwa sababu hawa watoto wanatuhitaji sisi," alisema.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE) wanawake, Tatu Mwenda, alitoa kwa serikali, kampuni na taasisi kuendelea kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum huku akiupongeza uongozi wa TCDC kwa kujitolea kuwasaidia watoto.

"Hiki kituo kinapokea watoto wadogo sana baada ya kupoteza wazazi wao wapo hadi wa siku tumeleta msaada ambao tunaamini ni mahitaji yao ya msingi kama vile pampasi za watoto, mchele, maharage, sabuni, sukari vyenye thamani ya Sh.milioni moja tumejaliwa hiki kidogo tumeleta na wengine walete tusaidie wapate mahitaji muhimu," alisema. Mlezi wa Kijiji cha Matumaini, Sister Christina Phidelis, alisema wamekuwa wakikutana na kero mbalimbali lakini wamekuwa wakizitatua kwa baadhi ya watu, taasisi na serikali.

Alisema kituo kinapokea watoto yatima wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na wamekuwa wakisimamiwa matumizi ya dawa na wengine tayari wamemaliza chuo na wana kazi.

"Hakuna kukata tamaa licha ya kwamba watoto hawa ni yatima lakini wanaishi kifamilia, wengine wenye moyo wa kujitolea wanakuja mtu na mume wake ambao pengine wameishakuwa na watoto wakubwa wanalea wale watoto yatima mnampa nyumba mnamgawia na watoto ili wapate malezi ya baba na mama na wanaenda mara moja kwa mwezi."

Alisema watoto wanaoishi katika kituo hicho wapo 147 mbali na ambao wapo Shule za Sekondari na Vyuo.

"Hapa kuna mtoto wa siku 18 ambaye aliletwa katika kituo baada ya mama yake kupata ugonjwa wa akili tunamhudumiwa vizuri, aliletwa akiwa na siku nane... mama yake alimtupa hivyo ndugu walishindwa jinsi ya kumsaidia wakaona mama wampeleke Mirembe na mtoto wamlete hapa sisi hatuwezi kukataa," alisema.





# Diwani atiwa mbaroni madai shambulio la aibu

**Grace Mwakalinga na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia viongozi wawili wa Kata ya Igaznzo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na mwananchi mmoja kwa tuhuma za kumshambulia kijana mmoja kwa kumtwanga makonde ndani ya ofisi ya serikali.

Viongozi wanaoshikiliwa ni Diwani wa Kata hiyo, Daniel William (35), Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iganzo, Erasto Mwankenja (48) na Mzee Henje Mbombo (74) ambaye ni mwananchi.

Wiki iliyopita video ya viongozi hao ilikuwa inazunguka kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha wakimshambulia kijana Shadrack Zakaria (28) ambaye ni mpigapicha wa mtaani.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, aliwaambia waandishi wa habari jana kwamba tukio la viongozi hao kumshambulia kijana huyo lilitokea Machi 3, mwaka huu, katika ofisi ya kata hiyo, mtaa wa Igodima.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni kwamba viongozi hao walikuwa wanamtuhumu kijana huyo kuwapiga picha bila ridhaa yao wakati wakifanya shughuli za maendeleo.

Pia alisema viongozi hao walikuwa wanamtuhumu kijana huyo kuwatolea lugha ya matusi wakati walipojaribu kumhoji kuhusu picha alizokuwa anawapiga.

"Mama mzazi wa kijana huyo, Esther Andrew, aliziba njia iliyokuwa inakatisha kwenye shamba lake na ndipo viongozi hao wakaamua kuifungua na kulima barabara. Sasa wakati wanaendelea na shughuli hiyo, ndipo kijana huyo aliamua kuwapiga picha," alisema.

"Lakini baadaye kijana huyo aliwafuata viongozi hao ofsini kwao kwenda kuwahoji sababu za kupitisha barabara kwenye eneo lao bila kuwashirikisha. Katika mazungumzo hayo, ndipo tukio la kushambulia lilianza," aliongeza.

Kamanda Matei alisema pamoja na kwamba mmiliki wa eneo hilo ambaye ni mama mzazi wa Zakaria alikosea kuziba njia, pia viongozi hao walifanya kosa kumshambulia.

Alisema viongozi hao walitakiwa kufuata utaratibu wa kisheria wa kusuluhisha jambo hilo badala ya kumpiga tukio ambalo alisema limeleta picha mbaya kwa wananchi dhidi ya ofisi za serikali.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, mama mzazi wa Zakaria ambaye ndiye alikuwa mmiliki wa eneo ilipopitishwa barabara, alisema alikuwa hajui kwamba mwanawe alishambuliwa kama ilivyokuwa ikionekana kwenye video.

Alisema alipata taarifa kwamba mtoto wake alikamatwa na kupelekwa katika Kituo Kikuu cha Polisi cha Mbeya na alifanya taratibu zote za kumtoa bila kujua kwamba alikuwa ameshambuliwa na viongozi hao.

"Machi 5 ambayo ilikuwa siku ya Jumamosi, nilitumiwa video ikionyesha mwanangu akipigwa utadhani ni mwizi au muuaji. Niliumia sana lakini sina namna," alisema Esther.

Alisema katika eneo hilo amekuwa na mgogoro na baadhi ya watu ambao wamekuwa wakichungia mifugo kwenye mazao yake na kila akiwashtaki kwa viongozi hao hawajawahi kuchukua hatua.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, baadhi ya bidhaa zilizokamatwa ambazo nyingine zimepigwa marufuku kuingia nchini na nyingine zimeingizwa kinyemele kutoka nchi jirani ya Zambia, baada ya kufanya operesheni juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanawake waliotoka gerezani sasa kunufaika na mikopo ya halmashauri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeziagiza halmashauri zote za mkoa huo kuwaingiza kwenye mkopo wa asilimia 10 wanawake wote wanaomaliza kutumikia vifungo vyao gerezani ili wautumie ujuzi walioupata kuanzisha shughuli za ujasiriamali.

Aidha, imeagiza kuundwa Kamati za Ulinzi na Usalama wa Wanawake na Watoto kwenye kila kata kukabiliana na matukio ya ukatili ambayo makundi hayo yamekuwa yakikabiliana nayo na kuyakwamisha kupata maendeleo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa maagizo hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo kimkoa yalifanyikia katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Homera alisema kwenye magereza yote wafungwa wanapatiwa mafunzo ya ufundi ambayo yanawasaidia kuwa na ujuzi wa kufanya shughuli za ujasiriamali, hivyo ili kuwaendeleza ni lazima wapewe mikopo.

Aliwataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi kusimamia jambo hilo ili litekelezwe katika kila eneo na kwamba litapunguza vitendo vya uhalifu kwenye jamii.

"Hili ni agizo ambalo watendaji wetu wa halmashauri lazima walisimamie kikamilifu. Kwenye magereza yetu kuna vyuo vya ufundi ambavyo vinatoa mafunzo ya ujasiriamali, hivyo naagiza wanawake wote wanaomaliza kutumikia vifungo wapewe mikopo," alisema Homera.

Pia aliwaomba viongozi wa dini na mila katika mkoa kusaidia kutoa elimu itakayosaidia kupunguza matukio ya watu kuuana kwenye jamii kwa sababu ya wivu wa mapenzi.

Homera alisema kwa sasa katika mkoa wa Mbeya huo, Jeshi la Polisi limefanya kazi kubwa ya kuzuia matukio hayo kwa kuwakamata watu wote wanaohusika kwenye matukio ya mauaji.

Alisema hivi karibuni walikamatwa watu waliodaiwa kumuua Mwenyekiti wa Mtaa wa Mwanyanje katika Kata ya Uyole pamoja na waliodaiwa kumuua Ofisa Ustawi wa Jamii wa Gereza la Watoto la Kabwe jijini Mbeya.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, alisema ofisi yake itaendelea kusimamia sheria ili kuhakikisha halmashauri zote za mkoa zinatoa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi maalumu.

Alisema kwa sasa katika mkoa wanawake wamekuwa wakijituma kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo zikiwamo biashara na kazi za kilimo na kwamba kundi hilo ndilo linaloongoza kwa uzalishaji.

# Waomba kukarabati miundombinu TAZARA

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi, imeombwa kufufua miundombinu ya njia za reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) iliyoko ndani ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) ili kurahisisha uingizwaji na kutolewa kwa mizigo.

Lengo la kuomba kufanya hivyo ni kupunguza msongamano wa magari na kuokoa bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi kama matunda.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Wasafirishaji Shehena Tanzania (TSC), Sallu Johnson, alitoa ombi hilo juzi kikao cha uhamasishaji kilichoandaliwa na Shirika la Wakala wa Huduma za Meli Tanzania (TASAC) na Taasisi ya Kiserikali ya Kikanda kwa Wanachama wa Jumuiya za Zambia, Kenya, Uganda na Tanzania kilichofanyika katika ukumbi wa Mkapa jijini hapa.

Alisema TPA imekuwa ikielemewa na shehena ya mizigo inayoingizwa kutoka maeneo mbalimbali nchini kwa kutumia magari makubwa ya mizigo, jambo linalosababisha msongamano mkubwa wa magari na kusababisha baadhi ya mizigo kukaa kwa muda mrefu bandarini huku meli wanazotarajia kusafirishia mizigo zikiwa zimeondoka bandarini.


"Ukifika pale Kurasini unaona kabisa foleni ya malori ni kubwa yakisubiri zamu pamoja na maandalizi ya nyaraka mbalimbali za kusafirisha shehena. Tunaiomba wizara husika kuboresha miundombinu ya reli ya TAZARA ili kuwaokoa Watanzania ambao wanapeleka bidhaa nje ya nchi na hasara wanazopata," alisema.

"Hivi ninavyoongea kuna shehena ya zao la chai imekwama bandarini na meli ambayo ilitarajia kusafisha ilishaondoka. Serikali ilione hili kwani usafiri wa reli ukiboreshwa utaondoka na hadha wanazokumbana nayo," aliongeza.

Johnson alisema kuna kila sababu ya kukaa kikao cha pamoja baina ya TPA na TAZARA ili kujadili suala hilo na kufika na makubaliano ambayo yatakuwa na tija kwa wasafirishaji.

"Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuna uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula la biashara hususan matunda ya parachichi, ndizi, mboga lakini changamoto ni namna ya kuzisafirisha kuingiza sokoni kwa kutumia usafiri wa reli na anga kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) kutokuwa na tija kwao," alisema Johnson.

Meneja wa Udhibiti wa Usafirishaji wa Njia ya Maji TASAC, Fatma Masenene, alisema lengo la mkutano huo ni kuhamasisha wasafirishaji wadogo kutumia usafiri wa meli kwa kuingiza mizigo ndani na nje kwa kutumia bandari nchini ikiwa ni pamoja na kusikiliza changamoto zao.



## HABARI ZANZIBAR

# Mwinyi alifumua Baraza Mawaziri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefanya mabadiliko katika Baraza lake la Mawaziri huku akiigawa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kutengeneza wizara mbili.

Katika mabadiliko hayo, mawaziri wawili wameenguliwa ambao ni aliyekuwa Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Abdallah Kombo na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Dk. Soud Nahoda.

Akitangaza mabadiliko ya baraza hilo juzi, Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Zena Ahmed Said, alisema Rais amewateua mawaziri wapya wanne, pia manaibu waziri saba.

Aliwataja mawaziri watakaounda baraza hilo ni Jamal Kassim Ali aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Masoud Ali Muhammed ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haroun Ali Suleiman ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Mudrik Ramadhan Soraga ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, wote wakibaki kwenye nafasi zao za awali.

Wengine walioteuliwa ni pamoja na Dk. Saada Salum Mkuya aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Awali alikuwa Waziri Nchi Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais.

Harusi Said Suleim ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kabla ya uteuzi huo alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Wete, Pemba.

Shamata Shaame Khamis ameteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni Pemba; Lela Muhammed Mussa ameteuliwa kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale na Simai Muhammed Said aliyekuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ameteuliwa kuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.

Tabia Maulid Mwita ameteuliwa kuwa Waziri wa Habari, Vijana, Sanaa, Utamaduni na Michezo (amebaki katika wizara hiyo); Rahma Kassim Ali ameteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi. Kabla ya uteuzi huo alikuwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi; Shaibu Hassan Kaduara ameteuliwa kuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini. Kabla ya uteuzi huo alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake.

Suleiman Masoud Suleiman ameteuliwa kuwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini; Nassor Ahmed Mazrui ameteuliwa kuwa Waziri wa Afya; Riziki Pemba Juma ameteuliwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii; Jinsia, Wazee na Watoto. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Omar Said Shabani ameteuliwa kuwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, akibaki katika wizara hiyo.

Hamza Hassan Juma ameteuliwa kuwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi. Kabla ya uteuzi huo alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo na Dk. Khalid Salum Muhammed ameteuliwa kuwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

## Serikali yajipanga ajira na uchumi wa ushindani

**Na Mwandishi Wetu,**

ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, amesema serikali ya Tanzania imekusudia kuwa na taifa lenye uchumi unaohimili ushindani wa kutoa ajira na mapato endelevu, usioharibu mazingira ili kufikia uchumi wa kidijitali.

Aliyasema jana hayo wakati wa ufunguzi wa semina ya uchumi wa kidigitali kwa mamlaka za juu za uamuzi wa sera nchini iliyofanyika Hoteli ya Marijan, Pwani Mchangani, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Katibu Mkuu Kiongozi alisema hatua hiyo inatokana na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayokusudia kuwa na taifa ambalo watu wake watakuwa na maisha bora, amani, utulivu na umoja.

Alisema mabadiliko na mageuzi hayo yanachochewa na utandawazi, ambao ni wimbi kubwa linaloonekana kuathiri maisha ya watu, maendeleo makubwa katika teknolojia yakibadilisha uchumi kuwa wa kidijitali.

Katibu Mkuu Kiongozi alisema uwapo wa mtandao wenye kasi kubwa, matumizi ya kompyuta zenye uwezo mkubwa zaidi, utunzaji takwimu, usalama wa mtandao, bidhaa na huduma za kisasa zinazopatikana katika mfumo wa TEHAMA ni vitu vilivyojenga uchumi wa kidigitali. Alisema utaratibu huo umeondoa mipaka ya ufikishaji wa bidhaa na huduma ambapo watu binafsi, wafanyabiashara na jamii wanaunganishwa katika muda mwafaka na kuifanya dunia ishirikiane zaidi.

Alifahamisha kuwa serikali itaipelekea Tanzania kufika kiwango cha juu zaidi cha uchumi na kwamba kuandaliwa kwa semina hiyo ni ushahidi wa serikali kufikia kiwango hicho.

Alisema mafunzo hayo yatanufaisha katika kuongeza kasi ya kuifikisha Tanzania kuwa katika kiwango cha juu cha uchumi wa kijiditali na kutegemea kunufaika kwa namna mbalimbali ikiwamo kuongezeka ubunifu katika shughuli za uzalishaji na kuongeza mapato.

Alibainisha kuwa katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, Tanzania ina dhamira ya kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu.


**EAGLE RECOVERIES LIMITED**

## TANGAZO LA NOTISI/MNADA

KWA NIABA YA NCBA BANK TANZANIA LIMITED WA S.L.P 20268, DAR ES SALAAM.TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA MDAIWA ALIYETAJWA HAPO CHINI ALIPE DENI LAKE ANALODAIWA KWA MUDA MREFU , ENDAPO ATASHINDWA KULIPA KWA MUDA ULIOTOLEWA DHAMANA YAKE ITAUZWA KWA RATIBA IFUATAYO.

| NA. | JINA LA MDAIWA | MALI INAYOUZWA | MAHALI ILIPO MALI INAYOUZWA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | ELIZABETH MKONY CHALO | NYUMBA YENYE HATI CT.113985, KIWANJA NA.281, KITALU NA." B" YENYE UKUBWA WA SQM 2,184 | ENEO LA TEGETA, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM (NYUMBA HII INAPAKANA NA BUDGET RESORT NA INATIZAMANA NA LAMI YA KUELEKEA BAHARI BEACH HOTEL/LEDGER PLAZA), | JUMANNE 29/03/2022 KUANZIA SAA 5 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mnada utafanyika sehemu ilipo dhamana.
3. Mnunuzi atakayefika bei ya juu atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei iliyofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya mnada
4. Endapo mteja atashindwa kumaliza 75% ndani ya siku 14 kiasi kilichotolewa awali 25% hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
5. Gharama za kubadilisha hati miliki (Transfer of ownsership) pamoja na gharama nyingine ni juu ya mnunuzi.

**Wote mnakaribishwa.**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**

**EAGLE RECOVERIES LIMITED,**
S.L.P 34462,
DAR ES SALAAM,
SIMU NA.0753 351 588/ 07683 152 822 /0743448888
EMAIL: eaglerecoveries2017@gmail.com

**MKURUGENZI MTENDAJI,**

**NCBA BANK TANZANIA LIMITED,**
S.L.P 20268,
AMANI PLACE,OHIO STREET
DAR ES SALAAM.
SIMU NA. +255 22 2125710
EMAIL: info@ncba.co.tz
WEB: www.ncbagroup.co.tz



PSSSF
Public Service
Social Security Fund

## TAARIFA KWA UMMA

Tunapenda kuwajulisha Wanachama wa PSSSF, Mfuko una ofisi tatu katika mkoa wa Dar es Salaam, hivyo Mwanachama atapata huduma yeyote anayoihitaji katika moja ya ofisi hizo, ikiwa pamoja na uhakiki wa Mstaafu.

Kwenda kuhudumiwa kwenye ofisi hizo tatu kutaondoa uwezekano wa Ofisi ya Ilala kuzidiwa na wastaafu wanaoenda kuhakikiwa.

Ofisi hizo ni;

1. **Ofisi ya kanda ya Ilala**, ipo Posta Mpya, mtaa wa Ohio katika jengo la PSSSF Golden Jubilee.
2. **Ofisi ya kanda ya Temeke**, ipo makutano ya mtaa wa Samora na Barabara ya Morogoro katika jengo la PSSSF House.
3. **Ofisi ya kanda ya Kinondoni**, ipo Makumbusho, barabara ya Ali Hassan Mwinyi katika jengo la PSSSF Millennium Towers.

Kwa taarifa zaidi piga simu ya bure namba **0800 110 040**

Leo. Kesho. Pamoja. 0800 110 040 www.psssf.go.tz PSSSF Watumishi_Pension PSSSFTZ

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 25 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late**
**MATRIDA MALUGU MKWABI**

By 1. MARIA ROBERT LIMBE
2. ……………………………..

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 17 day of 03 ..2022

**Dated at Morogoro this 18 day of 02 ..2022**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NDUGU EDWARD RICHARD KATUNZI anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T593AXR aina ya TOYOTA RAV 4, Rangi Pearly White yenye Chasis No. SXA117158475, Engine No.3S2703630 Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba ya Polisi DOD/DOD/RB/97696\/2022

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

DORIS ROBERT CHAGULA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 312 BCZ – DAIHATSU TERIOS. Chassis namba J100G024207. Engine namba HC724534. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: WMB/RB/216/2022.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLY ALLY AJIRANI**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya GARI(Noah) yenye namba za usajili **T 682 BNR** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0713745623**

**DSM /PHQ/RB/53590/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HALIMA SEIFU TUWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato che nne chenye index namba S.3841/0006 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **EPIPHANY SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/519052/2022.**

## KIWANJA KINAUZWA

KIWANJA KIPO KISUKURU SEGEREA JKT DSM, KINA UKUBWA WA MITA ZA MLABA (SQM) 2252, KIWANJA KIMEPIMWA NA KINA HATI, BEI NI MILIONI 55.

KWA MAWASILIANO PIGA 0754 857523/0655 857523.

## KUPOTEA KWA CHETI



John E. Kellya anatangaza kupotea kwa cheti Cha kidato cha nne,chenye Index no: S 1268-0168 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia Kisimiri secondary school November 2015. No ya cheti: CS15 0005830. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi. **DAR/CHU/RB/14657/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DOTTO SANGA CHRISTOPHER** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 599 CMA**. Engine namba **DF4HK1008497.** Chassis namba **MD625AF4XKIH08498.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MKB/RB/44/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAJABU S. ATHUMANI**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 841 CAH – TOYOTA NOAH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/TAN/RB/96777/2022.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 42 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**NZUMBI MWININGA MKWELLELA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY JUSTINA NORBERT KIHALI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 8 Day of APRIL, 2022
**Dated at Dodoma this 4TH day of March, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT
MAGISTRATE

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

## Viwanda vya dawa kuokoa bilioni 33/-

**Na Mary Geofrey,** MAKAMBAKO

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa viwanda vya dawa na vifaa tiba vilivyoko Idofi wilayani Makambako mkoani Njombe kutaipunguzia mzigo serikali wa kuagiza dawa nje ya nchi na kuokoa Sh. bilioni 33 kwa mwaka.

Mradi wa ujenzi wa viwanda hivyo vya Bohari ya Dawa (MSD) ulianza Oktoba 4, 2020 kwa gharama ya Sh. bilioni 16.7 na unatarajiwa kukamilika na kuanza kufanya kazi ndani ya miezi mitatu ijayo.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa MSD, Erick Mapunda, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Meja Jenerali Gabriel Mhidze, alisema mjini hapa juzi kuwa ujenzi huo umefika asilimia 90.

Alisema kukamilika kwa ujenzi huo kutafanikisha kuzalisha glovu 20,000 kwa saa, sawa na jozi 10,000 kwa saa. Alisema kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha dawa za vidonge vya rangimbili (Tablets) 330,000 kwa saa na vidonge vya kawaida (Capsules) 425,000 kwa saa.

"Dawa hizo ni Paracetamol, Amoxycillin, Arythromycin, Ampiclox ambazo zinahitajika kwa wingi nchini," alisema Mapunda.

Alisema kiwanda pia kitazalisha dawa za maji (syrup) chupa 180 kwa saa ambazo ni dawa za kikohozi, dawa za maumivu, cotrimoxazole syrup na Metronidazole syrup.

"Dawa nyingi ambazo zinatumika nchini zikiwamo za maumivu na antibayotiki na dawa za maji za watoto, zitazalishwa hapa Idofi na uzalishaji wa majaribio tayari umeshaanza na kuonyesha mafanikio makubwa," alisema Mapunda.

Mhandisi Msimamizi wa Mradi huo, Shiwa Mushi, alisema kwa sasa ufungaji wa eneo la usafi , vyoo vya ndani ya kiwanda pamoja na maeneo ya kubadilishia nguo unaendelea.

Alisema ghala la kuhifadhi malighafi linaloendelea kujengwa lina ukubwa wa mita za mraba 1,000 (urefu mita 50 na upana mita 20 na kimo mita sita).

# Waziri Kijaji ataja maeneo vipaumbele kwa wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imesema imeweka juhudi kuboresha mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji katika viwanda hasa katika maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ) na ya uzalishaji wa biadhaa kwa ajili ya kuuza nje (EPZ).

Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Dk. Ashatu Kijaji, alisema kuendeleza maeneo maalum ya SEZ na EPZ ni ya kipaumbele kwa serikali ikiwa na lengo la kuvutia wawekezaji wengi zaidi katika viwanda ili kutengeneza ajira nyingi na kuongeza pato la taifa.

Waziri Kijaji aliyasema hayo juzi wakati akitoa maelezo kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipotembelea Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) pamoja na kutembelea viwanda vilivyoko katika maeneo maalum ya kiuchumi la William Benjamin Mkapa.

Aliiambia kamati hiyo kuwa mkakati huo wa kuboresha mazingira ya uwekezaji unalenga kuunga mkono juhudi za dhati za Rais Samia Suluhu Hassan ya kuvutia wawekezaji wengi zaidi nchini na hasa kwenye sekta ya viwanda.

"Serikali imejizatiti kuweka miundombinu wezeshi katika maeneo yote ya SEZ na EPZ nchini ili kuwavutia wawekezaji wapya na kuchangia zaidi ukuaji wa uchumi," alisema.

Alisema kwa mfano katika maonyesho ya Dubai yaliyomalizika hivi karibuni, moja ya makubaliano yaliyosainiwa kati ya 36 ni ule wa kuwekeza katika maeneo ya SEZ na EPZ ikiwa ni moja ya juhudi za Rais Samia. Waziri Kijaji alihakikishia kamati hiyo kuwa wizara yake ipo katika hatua za mwisho kufanya kituo jumuishi cha pamoja (One Stop Centre) kuanza kuwahudumia wawekezaji na vibali vitaanza kupatikana ndani ya saa 24.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Daniel Sillo, aliipongeza Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa juhudi za kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi katika viwanda.

Aliitaka wizara iorodheshe changamoto mbalimbali zinazozuia uendelezaji wa maeneo ya SEZ na EPZ yaliyoko sehemu mbalimbali nchini.

Alisema lengo la kamati yake ni kuona kuwa changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi haraka iwezekenavyo kwa kushirikiana na karibu na serikali ili kuongeza kasi ya kuvutia wawekezaji nchini.

Naye Tarimba Abbas, mmoja wa wanakamati aliipongeza mamlaka ya EPZA kwa kazi nzuri ya kuvutia wawekezaji katika viwanda na akawataka kuongeza kasi Zaidi katika kuendeleza maeneo ya SEZ na EPZ ili kutengeneza ajira nyingi Zaidi kwa ajili ya vijana nchini.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, alisema miundombinu katika eneo la kiuchumi la William Benjamin Mkapa imekamilika kwa asilimia mia moja na maeneo mengine yapo katika hatua mbalimbali za awali.

Maeneo hayo ni pamoja na Bagamoyo SEZ, Kurasini SEZ, Manyara SEZ, Tanga SEZ, Bunda SEZ, Ruvuma SEZ na Manyoni SEZ. Alisema; "kwa sasa malengo ni kuendeleza maeneo mawili maalum ya kiuchumi ambayo ni Bagamoyo na Kurasini ambayo yameainishwa katika miradi ya kitaifa ya kimkakati (national flagship projects).




Balozi wa India nchini Tanzania Binaya Srikanta Pradhan (wa pili kulia), akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Jukwaa la Biashara la India nchini Tanzania, Gagan Gupta (kulia), Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongela (katikati), Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Afrika Mashariki, Salim Turkey (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Mkoa wa Arusha, Walter Maida, wakati wa kongamano la kujadili mambo mbalimbali ya sekta za kibiashara na uchumi hapa nchini, jijini Arusha hivi karibuni. **PICHA: UBALOZI WA INDIA**

# Kiwanda taulo za kike kujengwa Morogoro

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, ameazimia kuanzisha kiwanda cha kutengeneza taulo za kike ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hizo.

Msando alibainisha hayo juzi wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo kimkoa yalifanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Alisema tayari wameshaagiza mashine ya kutengeneza bidhaa hizo itakayoingia ndani ya mwezi huu na itakuwa chini ya usimamizi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Mariam Mtunguja.

Alisema kiwanda hicho kitakuwa cha kwanza kuanzishwa ndani ya mkoa ili kumsaidia mwanamke kwa kuwa kwa kiasi kikubwa wanawake wamekuwa hawapati ushirikiano linapokuja suala la hedhi salama.

Msando alisema hali hiyo imekuwa ikitengeneza dhana kwamba hedhi ni adhabu kwao na pia ni biashara kwa wanaume, akisisitiza ifike mahali wanaume wakubali suala la hedhi sio adhabu, bali limewafanya wanaume kuwa walipo.

Alisema asilimia 70 ya wanawake wanapambana na magonjwa katika mfumo wa haja ndogo kila mara wanapokwenda hospitalini kwa kuwa maji yaliyoko hayafai kufulia taulo za kike.

"'Tumfikirie mwanamke na magonjwa hayo, mwanamke anayelima kwenye shamba lake la mpunga anapata wapi taulo kwa ajili ya kujisitiri? Mwanamke anayekaa chini kuvuna mboga apate pesa ya kulisha familia yake, anapata wapi Sh. 8,000 za kununua taulo nzuri za kike?

"Mwanafunzi ambaye anakaa siku tatu hadi tano kwa ajili ya siku za hedhi, mwanamke ambaye leo hii anakata kipande chake cha khanga ili aweze kujistiri, tumfikirie mwanamke vizuri," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigela, aliahidi kuwasiliana na wizara husika kuona namna ya kuwapa nyongeza ya mikopo wanawake wanaokopa na kurejesha mikopo kwa wakati.

Alisema mikopo ya halmashauri imekuwa ikitolewa kwa makundi ya vijana, watu wenye ulemavu na kinamama lakini walio mstari wa mbele kurejesha na kwa wakati ni wanawake ambao katika kutikia wito huo wanahitaji kupata motisha ya kupewa nyongeza ya mkopo pale wanaporejesha kwa wakati.

Shigela alisema katika kudhihirisha hilo, Kikundi cha Moro Batiki kimefanikiwa kukopa Sh. milioni 100 kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, huku zaidi ya Sh. milioni 600 zikitolewa kwa wajasiriamali mbalimbali mkoani hapa kupitia mkopo wa NMB.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake, Agness Nabosa, alisema jamii inapaswa kutambua kuwa ili maendeleo endelevu yafikiwe, ushiriki wa wanawake na wanaume katika ngazi mbalimbali za uamuzi na shughuli za maendeleo ni muhimu.

Alisema jamii inatakiwa iwe na mtazamo kwamba wanawake wanao uwezo wa kutenda sawa na wanaume.

# BERKANE YAWASILI NCHINI KAMILI KUWAKABILI SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha RS Berkane ya Morocco kikitarajia kuwasili nchini leo, Simba imesema kikosi chake kimeingia kambini jana tayari kuendelea na maandalizi ya mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wageni hao kutoka Morocco.

Simba itaikaribisha RS Berkane katika mechi ya Kundi D itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally alisema viongozi, benchi la ufundi na wachezaji wa timu hiyo wamejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika mechi hiyo ambayo wanahitaji ushindi tu ili kujiimarisha kwenye msimamo wa kundi lao.

Ahmed alisema wanaahidi watapata matokeo mazuri, lakini akimtaja mchezaji majeruhi pekee aliyebaki katika kikosi chao ni Hassan Dilunga.

Alisema wanachama na mashabiki wa Simba wanatakiwa kuendelea kuungana ili ushindi huo wanaouhitaji upatikane, lakini wanafahamu wao watapambana kwa ajili ya kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

"Kikosi kinaingia kambini leo (jana) na mazoezi yanaanza rasmi kwenye Uwanja wa Mo Arena, taarifa tulizonazo RS Berkane watawasili kesho (leo), tunajua umuhimu wa mechi hiyo ambayo itakuwa ngumu, lakini kwa sababu tupo nyumbani na sisi tumejipanga kushinda," alisema Ahmed.

Kiongozi huyo aliongeza anaamini kila timu imejipanga kupata matokeo mazuri ikicheza nyumbani na kauli mbiu yao ni 'kila mtu ashinde kwake'.

Aliongeza wanafuraha kuona nyota wao, Denis Kibu na Thadeo Lwanga wamerejea kikosini na kitendo cha kuingia dakika 10 za mwisho katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Dodoma Jiji iliyochezwa juzi kimewaongezea nguvu huku akisema Jonas Mkude naye ameshakuwa sawa sawa.

Alikiri RS Berkane ndiyo timu bora zaidi kwenye kundi lao, lakini wamejipanga kuhakikisha ushindi unapatikana kwani hata kwenye mechi ya mwanzo ugenini, Februari 27, wachezaji walipambana licha ya hali ya hewa ya baridi kali kuwasumbua.

"Sisi tuliathiriwa na hali ya hewa, na wao wakija hapa watavuta pumzi ya moto. Nina maana hali ya hewa ya joto iliyoko jijini Dar es Salaam, ukitazama hali ya hewa ya Morocco ni baridi sana, na kwa sababu wachezaji wao wamezoea kucheza kwenye hali hiyo, itawawia vigumu mno kucheza kwenye hali ya joto, " kiongozi huyo alisema.




Wasanii wa Bendi ya Bahati wakitumbuiza katika sherehe ya kuchangia fedha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) na uzinduzi wa albamu ya The Orange iliyoandaliwa na kikundi cha muziki wa kizazi kipya cha Dada Hood. **PICHA: MTANDAO**

# *Shabiki Yanga ashinda M-BET*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI M-BET ikiwa imeshatumia Sh. milioni 226.5 kwa ajili ya zawadi kwa washindi wa Perfect 12, kampuni hiyo imemkabidhi shabiki wa Yanga na Chelsea, Peter Nangi kitita cha Sh.milioni 50, imefahamika.

Nangi ambaye ni mkazi wa Geita, ameshinda kiasi hicho cha fedha baada ya kubashiri kwa usahihi jumla ya michezo 12 ya mchezo wa kubahatisha wa Perfect12 wiki iliyopita.

Mkurugenzi Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi, alisema Nangi ameibuka mshindi ikiwa siku moja tu baada ya shabiki wa Simba wa Arsenal, Swalehe Enzi kujinyakulia zawadi ya Sh. milioni 176.4 kupitia pia Perfect 12.

" M-Bet sasa imeanzisha kampeni mpya inayoitwa ZALI LA M-BET ambapo ukicheza na M-Bet unaweza jishindia pikipiki na pesa taslimu kila wiki huku mwisho wa kampeni mshindi mmoja ataondoka na Toyota IST," alisema Mushi.

Kwa upande wake, Nangi alisema ushindi wake umetokana na kuwa makini katika kuchagua timu bila ya kufuata alama za ushindi ambazo kila timu inapewa katika mkeka.

Alisema alianza kushiriki mchezo huo miezi sita iliyopita na ushindi huu umempa faraja kwani ataongeza mtaji wake na kujishughulisha zaidi na kilimo.

"Siri kubwa ya kushinda bahati nasibu hii kujua uwezo wa timu pamoja na kufanyia utafiti wa timu, aina ya wachezaji ambao wamesajili, aina ya timu inayocheza nayo pamoja na majeruhi, ukibet kwa kupenda timu yako, unapotea kwani lazima uwe mfuatiliaji wa michezo mbalimbali," alisema Nangi.

# KMKM yaendelea kujiimarisha Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABAHARIA wa KMKM wameendelea kujiimarisha katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu baada ya kuitandika bila huruma Kisiwani ya Pemba mabao 5-1 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa juzi mchana.

Kwa ushindi huo, KMKM ambao ndio vinara wa ligi hiyo imefikisha pointi 48 ikifuatiwa na Maafande wa JKU wenye alama 41 na nafasi ya tatu inashikiliwa na Malindi yenye pointi 40.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema licha ya kuendelea kufanya vizuri katika ligi hiyo anakiri ushindani ni mkubwa kwa sababu kila timu imejipandaa vyema kusaka ushindi.

Msimu alisema uwepo wa zawadi kutoka kwa mdhamini kumechochea ushindani kwa sababu kila timu inahitaji kupata ubingwa na kujiepusha na janga la kushuka daraja.

Kocha huyo aliongeza timu zinazowania ubingwa zimeongezeka hivyo, hakuna ambaye mpaka sasa mwenye uhakika wa kutwaa taji hilo.

"Ligi inazidi kuwa ngumu kila kukicha, ugumu unakuja pale tunapokutana na timu ambazo zipo katika nafasi tatu za juu, majeruhi pia wanaongezeka, wachezaji wangu wanaumia sana kutokana na hali mzunguko huu wa lala salama," alisema Msimu.

Aliongeza amekuwa akiwasisitiza wachezaji wake kuongeza umakini katika kila mechi ili kuendelea kujiimarisha kwenye uongozi wa msimamo wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

KMKM itashuka tena dimbani keshokutwa kuvaana na JKU ikiwa ni mechi ya raundi ya 23 ya ligi hiyo ya juu visiwani hapa ambayo imebakisha mizunguko tisa ili kumalizika.

Bingwa wa ligi hiyo msimu huu atajinyakulia kitita cha Sh. milioni 50 kutoka PBZ na kupata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RUDIGER KUTUA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inataka kumsajili mlinzi wa Ujerumani, Antonio Rudiger wakati mkataba wa kiungo huyo wa Chelsea mwenye umri wa miaka 29 utakapomalizika mwisho wa msimu huu. (*Telegraph*)

### UNITED YAINGIA VITANI

MANCHESTER United pia wanapambana kutaka kumsajili mlinzi tegemeo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Antonio Rudiger ifikapo msimu huu wa joto. (*Express*)

### GNABRY AINGIA SOKONI

ARSENAL huenda wakajaribu kumsajili tena winga wa Ujerumani, Serge Gnabry kutoka Bayern Munich huku thamani ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26 aliyekuwa na washikabunduki hao kwa miaka minne. (*Football.London*)

### HAALAND AITAKA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund mwenye umri wa miaka 21, Erling Braut Haaland anataka kujiunga na Barcelona msimu huu wa joto. (*Sport*)

### KANE ATOA MSIMAMO

MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, amewaambia wachezaji wenzake atabakia Tottenham msimu ujao ikiwa watafuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya na kocha, Antonio Conte akabaki. (*Express*)

### SPURS YAMTAKA ROYAL

KLABU ya Tottenham Hotspur inajiandaa kupokea maombi ya kumnunua mlinzi mwenye umri wa miaka 23, Mbrazil Emerson Royal, chini ya mwaka mmoja baada ya kumnunua kwa pauni milioni 26 kutoka Barcelona. (*Sun*)

### ADEYEMI ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL watapata fursa ya kumsajili mshambuliaji wa Red Bull Salzburg mwenye umri wamiaka 20, Karim Adeyemi msimu wa joto dirisha la uhamisho litakapofunguliwa. (*Express*)

### GARNER ATAKIWA LEEDS

LEEDS United huenda wakawasilisha dau la kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United mwenye umri wa miaka 20, James Garner msimu wa joto, huku Southampton pia wakimfuatilia nyota huyo wa kimataifa wa England ambaye yuko Nottingham Forest kwa mkopo. (*Sun on Sunday*)

### EN-NESYRI MAMBO SAFI

ARSENAL na Newcastle United zinamtaka mshambuliaji wa Sevilla na Morocco mwenye umri wa miaka 24, Youssef En-Nesyri ambaye alihusishwa na uhamisho wa kuelekea Manchester United katika dirisha lililopita la Januari. (*Teamtalk*)

### ARTETA KUONGEZA NGUVU

NYOTA wa Real Sociedad ambaye ni raia wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22 na mchezaji wa kimataifa wa England na Everton, Dominic Calvert-Lewin (24), wametajwa ni walengwa wa Arsenal baada ya kocha, Mikel Arteta kusema hao ndio watakaopewa kipaumbele kipindi cha usajili wa majira ya joto. (*Sunday Express*)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LEWANDOWSKI AWEKA REKODI MPYA UEFA

## ●●● Afunga hat-trick na kuvunja rekodi ya Simone iliyodumu kwa miaka...

**MUNICH,** UJERUMANI

ROBERT Lewandowski aliweka historia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kufunga mabao matatu 'hat-trick' ndani ya dakika 23 za kipindi cha kwanza katika mechi ya pili ya hatua ya 16 bora dhidi ya Salzburg iliyochezwa Jumanne iliyopita.

Bayern Munich waliibuka na ushindi mnono wa mabao 7-1 na kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Lewandowski mchezaji wa kimataifa wa Poland aliweka rekodi ya kufunga mabao hayo matatu ndani ya dakika 23 na kujiwekea rekodi yake binafsi katika michuano hiyo.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kabisa katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mchezaji kufunga hat-trick ndani ya dakika 23 za mwanzo, akiipiku rekodi ya Marco Simone aliyefunga mabao matatu dani ya dakika 24 akiwa na Milan dhidi ya Rosenborg mwaka 1996.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 aliwaweka wababe hao wa Bavaria mbele kwa mkwaju wa penalti dakika ya 12 baada ya kufanyiwa faulo na Maximilian Wober.

**Alitumia mkwaju wa pili kwenye kona ya chini kushoto katika dakika ya 21 kufunga bao la pili na la tatu alifunga kwa paja baada ya mpira wake kumpita kipa, Philipp Kohn.**

Hiyo ilikuwa ni hat-trick ya tano kwa Lewandowski katika historia ya mashindano hayo, akizidiwa na Cristiano Ronaldo na Lionel Messi (wote wakifunga mara nane).

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,013

MECHI KALI
LEEDS
VERSUS
ASTON VILLA
1 | 2.66
X | 3.51
2 | 2.51

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MODRIC AMTAKA MBAPPE MADRID




**MADRID,** Hispania

LUKA Modric anatumaini, Kylian Mbappe atajiunga naye Real Madrid msimu ujao.

Mkataba wa Mbappe unamalizika mwishoni mwa Juni na fowadi huyo wa Paris Saint-Germain anaendelea kuhusishwa na kutaka kuhamia Madrid.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 alijumuishwa kwenye kikosi cha PSG kilichominyana na Los Blancos jana Jumatano katika mechi ya pili ya hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mbappe ndiye aliyekuwa tofauti katika mechi ya kwanza, akifunga bao la ushindi dakika za lala salama na kuwapa PSG faida ya 1-0 baada ya Lionel Messi penalti yake kuokolewa na kipa wa Madrid, Thibaut Courtois.

Modric pia anakaribia mwisho wa mkataba wake, lakini amezungumzia nia yake ya kuongeza muda wake wa kukaa na vinara hao wa LaLiga Madrid, na mshindi huyo wa Ballon d'Or 2018 amesema mchezaji yeyote duniani angemtaka Mbappe awe mchezaji mwenzake.

"Tunataka kucheza na wachezaji wakubwa, Kylian ni mmoja wa hao. Bila shaka, ningependa kucheza naye, tuone," kiungo huyo aliwaambia waandishi wa habari.



# 'Kipigo Inter kimeiamsha Live'

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah amesema kufungwa kwa Liverpool 1-0 na Inter Milan katika mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye hatua ya 16, kutakuwa kama "simu" ya kuwaamsha ili wajitume zaidi kwa ajili ya kutinga fainali.

Wakiwa wanaongoza 2-0 katika mechi ya kwanza kutokana na mabao ya Roberto Firmino na Salah dakika za lala salama, Wekundu hao walionekana kustarehe katika saa ya kwanza ya mechi ya marudiano iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Anfield.

Lakini bao la kwanza la Lautaro Martinez kwenye mashindano hayo tangu Novemba mwaka juzi, liliwapa Inter matumaini makubwa ya angalau kulazimisha muda wa ziada.

Kadi nyekundu ya Alexis Sanchez sekunde 107 baadaye ilionekana mbaya, ingawa, Inter ilishindwa kutengeneza nafasi nyingine za wazi.

Kipigo hicho ni cha kwanza kwa Liverpool katika dimba la Anfield katika michuano yote tangu Machi 7, mwaka jana.

Lakini kwa kuwa timu yake imefanya vya kutosha kuendeleza ushindi wa 2-1 kwa jumla, Salah ana matumaini ya kutumia kipigo hicho kama ishara ya kuwaamsha.

## HABARI MICHEZO


3,643,920

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/03/22 | 18:00 | Millwall vs Middlesbrough | 2.22 | 3.20 | 3.15 |
| 02. 12/03/22 | 18:00 | Coventry vs Sheffield Utd | 2.60 | 3.14 | 2.65 |
| 03. 12/03/22 | 18:00 | Blackpool vs Swansea | 2.36 | 3.29 | 2.85 |
| 04. 12/03/22 | 19:00 | Montpellier vs Nice | 3.02 | 3.47 | 2.24 |
| 05. 12/03/22 | 23:00 | Troyes vs Nantes | 2.63 | 3.22 | 2.68 |
| 06. 12/03/22 | 23:00 | Getafe vs Valencia | 2.46 | 3.06 | 3.06 |
| 07. 12/03/22 | 23:30 | Belenenses vs Boavista | 2.71 | 3.25 | 2.51 |
| 08. 13/03/22 | 14:15 | Fortuna Sittard vs Willem II Tilburg | 2.80 | 3.35 | 2.48 |
| 09. 13/03/22 | 15:00 | Luton Town vs QPR | 2.25 | 3.20 | 3.10 |
| 10. 13/03/22 | 15:30 | Hannover vs Nurnberg | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 11. 13/03/22 | 17:00 | Angers vs Reims | 2.27 | 3.13 | 3.28 |
| 12. 13/03/22 | 17:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.37 | 3.32 | 2.92 |
| 13. 13/03/22 | 17:00 | Everton vs Wolverhampton | 2.29 | 3.26 | 3.16 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 10/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1218 | Artsakh vs Pyunik Yerevan | 3.90 | 3.60 | 1.90 |
| 14:00 | 2286 | FC Noravank vs Ararat Armenia | 11.00 | 6.00 | 1.24 |
| 16:00 | 2143 | Shabab AL Khaleel vs Jabal EL Mokaber | 2.06 | 3.35 | 3.65 |
| 16:00 | 2683 | Buildcon vs Kabwe Warriors | 2.37 | 2.80 | 3.55 |
| 16:00 | 3191 | Mosaset AL Bireh vs Tubas | 2.23 | 3.30 | 3.25 |
| 16:30 | 3629 | Persija Jakarta vs Pusamania Borneo | 2.77 | 2.86 | 2.57 |
| 16:45 | 2199 | Baniyas vs Al Nasr Dubai | 2.94 | 3.23 | 2.22 |
| 17:00 | 1539 | AL Arabi vs Al Fehaheel | 1.38 | 4.62 | 6.35 |
| 17:00 | 3127 | Lekhwiya SC vs Al Ahli Doha SC | 1.08 | 8.87 | 16.39 |
| 17:00 | 4493 | NK Aluminij vs Maribor | 4.83 | 3.87 | 1.58 |
| 18:25 | 2910 | Al Fateh (KSA) vs Abha | 2.04 | 3.71 | 3.22 |
| 18:50 | 3647 | Al Taawon vs Al Faisaly (KSA) | 1.82 | 3.70 | 4.20 |
| 19:10 | 2322 | Umm-Salal SC vs Al Arabi Doha SC | 3.23 | 3.52 | 1.98 |
| 19:15 | 5197 | Al Sharjah SC vs Ajman Club | 1.48 | 4.16 | 5.42 |
| 19:30 | 1873 | Al Kuwait SC vs Al Salmiyah | 1.68 | 4.10 | 4.60 |
| 19:30 | 3056 | NK Mura vs Olimpija Ljubljana | 2.46 | 3.09 | 2.70 |
| 20:15 | 1413 | Budafoki Mte vs Kecskemeti TE | 3.75 | 3.60 | 1.94 |
| 20:30 | 5560 | AFC Unirea Constanta vs Petrolul Ploiesti | 8.12 | 4.74 | 1.31 |
| 20:45 | 2854 | Partizan vs Feyenoord | 3.29 | 3.19 | 2.26 |
| 20:45 | 2914 | PAOK vs KAA Gent | 2.25 | 3.15 | 3.35 |
| 20:45 | 3760 | Sevilla FC vs West Ham | 2.11 | 3.14 | 3.74 |
| 20:45 | 4476 | Vitesse Arnhem vs Roma | 3.64 | 3.64 | 1.96 |
| 20:45 | 5915 | Slavia Prague vs LASK Linz | 1.76 | 3.76 | 4.41 |
| 21:30 | 3936 | Blumenthaler SV vs SFL Bremerhaven | 2.22 | 4.25 | 2.41 |
| 21:30 | 5022 | TUS Haltern vs SV Schermbeck 1912 | 3.32 | 4.05 | 1.81 |
| 21:30 | 5039 | SV 1914 Eilendorf vs Fortuna Koln II | 2.65 | 4.04 | 2.11 |
| 22:00 | 1310 | SV 1910 Breinig vs FC Pesch | 2.85 | 4.50 | 2.05 |
| 22:00 | 3777 | Breidablik Kopavogur W vs KR Reykjavik W | 1.05 | 13.00 | 35.00 |
| 22:00 | 4018 | Throttur Reykjavik W vs Keflavik W | 2.95 | 4.00 | 2.13 |
| 22:00 | 4070 | Stjarnan vs Breidablik | 3.00 | 4.50 | 1.99 |
| 22:00 | 5094 | Fylkir vs Hafnarfjordur | 2.65 | 4.04 | 2.11 |
| 22:00 | 5663 | Viktoria Arnoldsweiler vs 1. FC Duren | 9.70 | 6.59 | 1.18 |
| 22:30 | 4463 | Wolverhampton vs Watford | 1.82 | 3.36 | 4.72 |
| 22:30 | 4540 | Norwich City vs Chelsea | 10.00 | 5.40 | 1.29 |
| 22:30 | 5792 | Southampton vs Newcastle | 1.96 | 3.64 | 3.64 |
| 22:45 | 4294 | Leeds vs Aston Villa | 2.66 | 3.51 | 2.51 |
| 23:00 | 1114 | PSV Eindhoven vs Copenhagen | 1.50 | 4.28 | 6.18 |
| 23:00 | 1270 | Sporting Braga vs Monaco | 2.80 | 3.21 | 2.55 |
| 23:00 | 1434 | Barcelona vs Galatasaray | 1.19 | 6.61 | 14.78 |
| 23:00 | 2835 | Fortaleza Ceif FC vs Independiente Santa Fe W | 10.65 | 6.00 | 1.19 |
| 23:00 | 3082 | Leones FC vs Real Cartagena | 1.54 | 3.87 | 5.22 |
| 23:00 | 3596 | Marseille vs FC Basel | 1.62 | 4.01 | 5.22 |
| 23:00 | 3677 | Bodo Glimt vs AZ Alkmaar | 2.81 | 3.46 | 2.41 |
| 23:00 | 3787 | Leicester vs Rennes | 2.07 | 3.65 | 3.30 |
| 23:00 | 4315 | Rangers vs Red Star Belgrade | 1.74 | 3.66 | 4.71 |
| 23:00 | 5144 | CD Deportes Tolima Sa vs CA Bucaramanga Sa | 1.39 | 4.50 | 8.60 |
| 23:00 | 5285 | Atalanta vs Bayer Leverkusen | 1.97 | 3.60 | 3.65 |
| 23:00 | 5811 | Orsomarso vs Barranquilla FC | 2.16 | 3.00 | 3.29 |
| 23:30 | 2887 | Club Cortulua vs Union Magdalena SM | 1.95 | 3.18 | 3.67 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MANULA, DIARRA WAONGOZA KWA 'CLEAN SHEETS' LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Simba, Aishi Manula na Djigui Diarra wa Yanga wanaongoza kwa kucheza mechi nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara bila kuruhusu nyavu zao kutikiswa maarufu kama 'clean sheets'.

Manula ambaye kipa chaguo la kwanza wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) na Diarra ambaye ni kipa wa kimataifa kutoka Mali wote hawajaruhusu bao kwenye mechi tisa ambazo wamekaa langoni.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Bodi ya Ligi Tanzania, Manula na Diarra wakiwa na 'clean sheets' tisa kila mmoja, kipa mwingine wa Yanga, Abuotwalib Msherry anafuatia akiwa hajafunga bao lolote katika michezo nane.

**Hata hivyo, 'clean sheets' zake zinahesabiwa na zile alizotoka nazo Mtibwa Sugar ambapo aliichezea mwanzoni mwa msimu, kabla ya kipindi cha dirisha dogo la usajili.**

Makipa wengine wanaofuatia kwa kufanya vyema, wakisimama langoni ni Metacha Mnata wa Polisi Tanzania ambaye amekaa langoni na kutoruhusu wavu wake kuguswa kwenye mechi sita sawa na Mussa Mbisa wa Coastal Union.

Wenye 'clean sheets' tano mpaka sasa ni Ahmed Salula wa Azam FC na James Seetuba wa Biashara United, huku makipa Deogratius Munishi "Dida" , Haroun Mandanda wote wa Mbeya City, Hussein Masalanga (Dodoma Jiji), Jonathan Nahimana (Namungo) na Juma Kaseja wa KMC, wote wana 'clean sheets' nne kila mmoja.

Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo mdhamini wake mkuu ni Benki ya NBC imeingia katika mzunguko wa pili na vinara ni Yanga yenye pointi 42.




Viongozi wa Chama cha Soka cha Mpira wa Miguu wa Wanawake Nchini (TWFA), wakiwa pamoja na wawakilishi wa Global Peace Foundation, UN Women, Women Trust Fund na Ilala Queens ambao waliibuka 'Malkia wa Wanawake 2022' katika mechi za kirafiki zilizochezwa juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

# *Njau afunguka kilichombeba*

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA na mwamuzi wa ngumi wa kimataifa hapa nchini, Pendo Njau amesema siri ya mafanikio yake ni uvumilivu pamoja na nidhamu kwa makocha wote waliokuwa wanamfundisha.

Njau aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam baada ya kupokea tuzo iliyotolewa katika Siku ya Wanawake Duniani na kusema amefurahi sana kwa heshima ambayo aliipata hapo juzi.

Mwamuzi huyo alisema hiyo ni tuzo yake ya kwanza kupata tangu alipoanza mchezo huo na itampa nguvu ya kuendelea kufanya vyema majukumu yake.

"Siri ya mafanikio mpaka hapa nilipofika ni umakini na kazi yangu pamoja na uvumilivu niliokuwa nao, bila nidhamu huwezi kufika popote," alisema Njau.

Aliongeza anapitia changamoto mbalimbali anapochezesha mapambano kwa sababu tu ya kuwa mwanamke, lakini anapambana nazo na hatimaye anatekeleza majukumu yake kwa weledi.

Alitaja baadhi ya changamoto anazokutana nazo ni kusumbuliwa kimapenzi jambo ambalo amewataka wanamichezo wengine wanawake wasikubali kujirahisisha ili kujiepusha na maradhi.



Michezo
Alhamisi Machi 10, 2022
Nipashe



Lewandowski aweka rekodi UEFA UKURASA 21



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza mubashara kupitia simu na Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, wakati wa kuchangia fedha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), inayotakiwa kujiandaa na mashindano mbalimbali ya kimataifa. Zaidi ya Sh. milioni 370 zilichangwa katika hafla hiyo. **PICHA: BMT**

## Yanga hakuna kulala

**Na Adam Fungamwango**

ILI kuhakikisha makali ya wachezaji yanaendelea, Yanga inatarajia kucheza mechi ya kirafiki ambayo inalenga kuwaongezea utimamu wa mwili nyota wake lakini ikiweka wazi straika wao tegemeo, Fiston Mayele ataanza mazoezi na kikosi hicho leo.

Yanga imeamua kusaka mechi ya kirafiki baada ya kuwa na siku 10 za mapumziko tangu ilipomaliza mchezo wake dhidi ya Geita Gold FC wiki iliyopita.

Msemaji wa Yanga, Haji Manara aliliambia gazeti hili wako katika hatua za mwisho za mazungumzo na timu watakayocheza nayo kwa ajili ya kutimiza maombi ya benchi la ufundi.

"Tuko kwenye kiwango cha juu sana hivi sasa, kwa hiyo hatuwezi kukaa wiki nzima ikapita hivi hivi bila wachezaji wetu kupata mechi, na hata wale ambao hawajacheza mechi yoyote nao wapate angalau dakika fulani za kucheza. Mara nyingi wachezaji wakikaa muda mrefu bila kucheza wakirudi ni kama wanaanza upya," alisema Manara.

Aliongeza Yanga itaingia kambini leo kujiandaa na mechi hiyo ya kirafiki pamoja na mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC utakaochezwa Machi 16, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Hata hivyo nyota wa Yanga jana asubuhi walifanya mazoezi ya gym chini ya Kocha Msaidizi, Cedrick Kaze.

"Leo (jana), tumeanza kufanya mazoezi ya gym, wachezaji wote wanaendelea vizuri na tumeanza na mazoezi haya ili kuwaweka sawa," alisema Kaze.

# Simba yakoleza makali

**Na Saada Akida**

## ●●● Ni kwa ajili ya kuivaa Berkane, Rais Samia aongoza kuichangia Twiga...

WAKATI Simba ikijiweka imara kwa ajili ya kuwakaribisha RS Berkane kutoka Morocco, Rais Samia Suluhu Hassan juzi aliongoza harambee ya kuichangia fedha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), ili iweze kujiandaa vyema na mashindano mbalimbali ya kimataifa.

**Simba itawakaribisha RS Berkane katika mechi ya Kundi D ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.**

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema jana kikosi cha timu yao kimeshaingia kambini kuendelea na maandalizi ya mchezo huo ambao wanahitaji kupata ushindi na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Maandalizi ya mchezo yanaendelea vyema na tayari viingilio vya mchezo vimetangazwa mapema ili mashabiki wanunue tiketi kupitia njia ya mitandao na vituo, wanunue tiketi mapema ili kuepuka usumbufu siku ya mchezo," alisema Ahmed.

Meneja huyo alisema wanajivunia kuwapo kwa wachezaji wanaojua nini wanatakiwa cha kufanya katika mechi hiyo hasa wanapokuwa kwenye uwanja wa nyumbani katika mashindano hayo ya kimataifa.

"Ukiangalia kundi letu unaona jinsi gani kuna umuhimu wa kushinda nyumbani, wachezaji wana morali na hali ya kushinda hii mechi kwa sababu tunahitaji kupata pointi tatu," alisema meneja huyo.

Aliongeza pia Simba iko katika hatua nzuri za mazungumzo ya kumsajili kiungo mshambuliaji wa US Gendarmerie, Mnigeria, Victorien Adebayor kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya Kimataifa.

"Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', tayari ameanza kufanyia kazi suala hilo la kuwasiliana na meneja wake na tumeelezwa kuna timu Denmark pia inahitaji huduma ya nyota huyo, lakini mchezaji mwenyewe alieleza wazi yuko tayari kutua ndani ya klabu yetu," alisema Ahmed.

Aliongeza mechi yao itachezwa kuanzia saa 10:00 jioni na wanaamini muda huo utakuwa na faida kwao kutokana na hali ya hewa ya joto ambayo itakuwa ni mateso kwa wapinzani wao, RS Berkane waliozoea mazingira ya baridi.

"Sisi tulipata tabu hali ya hewa ya Morocco, nina imani hata wao watakutana na kile tulichokutana nacho kwao, watavuta pumzi ya moto, tunawaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi uwanjani kwa ajili ya kuwapa presha wapinzani wetu hao," Ahmed alisema.

Wakati huo huo, zaidi ya Sh. milioni 300 zinatarajiwa kukusanywa kuichangia Twiga Stars huku Rais Samia akiahidi kutoa kaisi cha Sh. milioni 15.

"Nafuatilia matukio na kuona watu wengi wanachangia na kuwapongeza zoezi hilo, limenishawishi nachangia Sh. milioni 15, rai yangu fedha hizo zinazokusanywa ziwafikie walengwa na kufanyia kazi iliyokusudiwa ya kusaidia timu hiyo ili iendelee kupeperusha bendera ya Taifa vizuri," alisema Rais Samia.

Naye mgeni rasmi katika harambee hiyo, Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, alisisitiza fedha hizo zitasimamiwa na kutumika katika malengo yaliyokusudiwa kwa ajili ya kuhakikisha wanawake wanafikia malengo.

"Tukiangalia kwa miaka ya hivi karibuni tunaona jinsi wanavyopambana na kuletea heshima taifa letu, ningependa hata timu zetu za wanaume kuchukuwa video za wenzetu kuona jinsi gani wanavyofanikiwa kuleta heshima nchini kwetu," alisema Nchemba.

Mbali na ahadi za fedha, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Henry Tandau, alisema kamati yao itaisaidia timu hiyo maandalizi na kuhakikisha inapata tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki ya mwaka 2024, ambayo itafanyika jijini Paris, Ufaransa.

"Tumechangia kiasi ya Sh. milioni tano, ila hatuishii hapo tu, tutakutana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ili kuangalia namna ya kupata kocha mwenye kiwango cha juu ili kuisaidia timu," alisema Tandau.

Serikali pia ilikabidhi hati za viwanja ambavyo wachezaji wa Twiga Stars walipewa zawadi na Rais Samia mwaka jana baada ya kutwaa ubingwa wa COSAFA.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >